epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumanne Aprili 2, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581634
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

**Chanzo** kukatika umeme nchini chatajwa

UKURASA 3



**Ziwa** Tanganyika kufungwa kwa miezi mitatu

UKURASA 8



MAKALA MAALUM

**Ilivyo** hatari Tril. 9.4/- za serikali kupotea

UKURASA 18



UKURASA 21

**'UBINGWA EPL HAUPO MIKONONI MWETU'**




# Mauaji yarindima sikukuu ya Pasaka

• **Baba** adaiwa kumnyonga mwanawe apate michango ya kikundi; matukio tofauti ya mapanga yahitimisha uhai wa mwanasheria, mwalimu na mwanafunzi...*Endelea ukurasa 5*

# Majina matatu yatawala kiti cha Mwenezi wa CCM

UKURASA 2



Lengai Ole Sabaya | John Mongella | Amos Makalla

**MICHEZO** BENCHIKHA ATAJA MBINU KUISHIKA AL AHLY UK.24
**KATUNI** UK.6

# Majina matatu yatawala kiti cha Mwenezi wa CCM

**Na Mwandishi Wetu**

LEO ni miaka mitatu na siku 14 tangu Rais Samia Suluhu aingie madarakani. Uteuzi na utenguzi wake wa viongozi umekuwa unatikisa serikalini na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Ndani ya uongozi wake, kumekuwa na mabadiliko ya mara kwa mara ya uongozi ndani ya CCM, huku nafasi ya Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo ikiguswa karibu kila yanapofanyika.

Katika kipindi hicho cha miaka mitatu, makada watatu wa chama hicho wameteuliwa kushika nafasi hiyo, lakini hakuna aliyedumu. Kiti hicho kwa sasa kiko wazi baada ya Paul Makonda kuteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa katika mabadiliko yaliyotangazwa usiku wa manane kuamkia Jumapili ya Pasaka.

Ni mabadiliko yaliyoibua hisia tofauti huku kukiwa na minong'ono kwa wanaotajwa kushika nafasi hiyo. Wakuu wa Mikoa waliotenguliwa usiku wa kuamkia Pasaka, John Mongella na Amos Makalla pamoja na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya wanatajwa kuwa na nafasi ya kukalia kiti cha Katibu wa Uenezi CCM.

Rais Samia aliapishwa kuwa Rais wa sita wa Tanzania Machi 19, 2021 kufuatia kifo cha Rais wa Tano, Dk. John Magufuli kilichotangazwa Machi 17, 2021. Mnamo Aprili 30, 2021, Halmashauri Kuu ya CCM katika kikao maalum ilipitisha kwa kauli moja Rais Samia kuwa mgombea pekee wa nafasi ya Mwenyekiti wa CCM Taifa.

Wakati huo, Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Humprey Polepole ndiye aliyeujulisha umma juu ya uamuzi huo, na Mkutano Mkuu Maalum ulipitisha Samia kuwa Mwenyekiti wa CCM Taifa, akichukua nafasi ya Hayati Dk. Magufuli.

Mara baada ya kuingia madarakani, mwenyekiti huyo alianza kuisuka safu ya uongozi ndani ya chama hicho, kwa kumteua Daniel Chongolo ambaye kabla alikuwa Mkurugenzi wa Mawasiliano chini ya Idara ya Itikadi, Uenezi na Mafunzo ikiwa chini ya Nape Nnauye, akitokea kwenye nafasi ya Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni.

Halmashauri Kuu pia ilimteua Christina Mndeme kuwa Naibu Katibu Mkuu Bara huku Abdalah Juma Sadala akiendelea kuhudumu nafasi hiyo upande wa Zanzibar.

Pia nafasi ya Polepole aliyoitumikia tangu Desemba 13, 2016 akijaza nafasi iliyoachwa wazi na Nape, ilikabidhiwa kwa Shaka Hamdu Shaka huku Katibu wa Uchumi na Fedha akiwa Frank Hawasi.

Ikumbukwe kuwa Polepole aliteuliwa na Rais Magufuli kuwa mbunge Novemba 29, 2020. Aprili 14, 2022, Rais Samia alimteua Polepole kuwa Balozi wa Tanzania nchini Malawi na mwaka uliofuata, alimhamishia Cuba ambako yuko hadi sasa akihudumu katika nafasi hiyo.

Shaka alidumu kwenye nafasi hiyo kwa mwaka mmoja na miezi minane na siku 13, hadi Januari 14, 2023, Halmashauri Kuu ya CCM ilipomteua Sophia Mjema kuwa Katibu wa Itikadi na Uenezi, huku Rais Samia akimteua Shaka kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kilosa ambako anahudumu hadi sasa.

Mjema alidumu kwenye nafasi hiyo kwa miezi tisa na siku nane, kisha Paul Makonda kuteuliwa na Halmashauri Kuu kushika wadhifa huo aliodumu nao kwa siku 162, akiteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha.

Chongolo, akiwa ni Katibu Mkuu wa CCM wa 11 alijiuzulu nafasi hiyo baada ya kashfa mbalimbali alizohusishwa na kusambazwa kwenye mitandao ya kijamii. Machi 9, mwaka huu aliteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Songwe.

Chongolo alidumu kwenye nafasi hiyo kwa miaka miwili miezi minane na siku 15, kisha Halmashauri Kuu baada ya kuridhia barua ya kujiuzulu ya Chongolo ilimteua Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi kushika wadhifa huo anaoendelea nao hadi sasa.

Katika kipindi hicho, Sekretarieti ya CCM imekuwa inapitia mabadiliko mbalimbali ambapo hivi karibuni, Rais Samia alimteua aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu CCM Bara, Anamringi Macha, kuwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga.


Kati ya waenezi waliopita chini ya uenyekiti wa Rais Samia, Makonda ndiye aliyedumu kwa muda mfupi zaidi, huku kukiwa na mjadala kwenye mitandao ya kijamii kuwa kupewa kwake nafasi ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha ni kupanda ngazi au kushuka ngazi huku kukiwa na maswali mengi ya kilichosababisha kuondolewa katika Sekretarieti ya CCM licha ya kuonekana kufanya vizuri kwenye ziara zake mikoani kuimarisha chama.

Katiba mabadiliko ya juzi, mbali na Makonda, Rais alimteua Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM), Fakii Lulandala kuwa Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, huku Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi CCM, Gilbert Kalima akiteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Mkinga.

**WANAOTAJWA**

Kwenye makundi sogozi ya WhatsApp na mitandao mingine ya kijamii, majina ya viongozi watatu yameonekana kutawala mijadala ya wanaotajwa kuwa na nafasi kubwa ya kurithi mikoba ya Makonda ndani ya Sekretarieti ya CCM.

Katika mjadala huo, taarifa ya Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Zuhura Yunusi, inarejewa kwa kuangalia majina ya viongozi ambao uteuzi wao umetenguliwa, lakini kukawa na maelezo kwamba watapangiwa majukumu mengine.



Katika taarifa hiyo wapo ambao wameelezwa uteuzi wao umetenguliwa, lakini aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mongella na yule wa Mwanza, Makalla ilielezwa watapangiwa kazi nyingine.

**AMOS MAKALLA**

Ana mambo yanayoshabihiana na Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, kuanzia uswahiba wa masomoni IDM Mzumbe, wana umri unaofanana, miaka 52 na kihistoria ni makada kindakindaki waliokulia kwenye chama, hata wakawa vigogo wa UVCCM wakiwa na nyendo za kisiasa pamoja.

Walitumikia pamoja kwenye uongozi wa UVCCM chini ya Mwenyekiti Nchimbi kisha baadaye walipokomaa kisiasa na umri, wakapitia vyeo tofauti, Makalla wakati fulani akirejeshwa kwenye Sekretarieti ya CCM, akiwa kwenye Idara ya Fedha, kama alivyotumikia UVCCM.

Mwenzake Nchimbi akazungukia kwenye utendaji wa kiserikali zaidi, akianzia Baraza la Taifa la Uhifadhi wa Mazingira (NEMC) iliyokuwa ajira yake ya kwanza, hata akakwea kwenye ukuu wa wilaya, ubunge uliompa uwaziri na baadaye akiibukia balozi katika nchi kadhaa kabla ya kurejea tena katika chama.

Mizunguko kama hiyo ilikuwa kwa Makalla, kuna wakati hakuonekana katika nafasi hizo, ubunge na kisha Naibu Waziri (Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, pia Maji na Umwagiliaji) kabla ya kurejea tena kwenye ukuu wa mkoa na sasa rasmi kuna tetesi za kurejea tena sebuleni katika chama wakiwa makada walioiva kama ilivyomtokea swahiba wake Nchimbi.

Hata kitaaluma, wana-Mzumbe hao, Balozi Nchimbi ambaye ngazi yake ya kwanza kitaaluma ni utawala wa umma, Makalla amezama kwenye uhasibu, lakini kwa pamoja waliporejea shuleni, shahada zao za pili ni za usimamizi wa biashara, unasaba wao na Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia, naye ni mwana-Mzumbe wa darasa moja na Balozi Nchimbi, lakini kamtangulia kwa miaka mingi.

**OLE SABAYA**

Mbali na Makalla na Mongella, orodha ya wanaotajwa kurithi mikoba ya Makonda pia ina jina la Ole Sabaya, mzaliwa wa Sambasha, Arumeru, mkoani Arusha mwaka 1986, ambaye anatoka familia ya kifugaji ya Loy Thomas Sabaya ambaye kwa sasa ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Arusha.

Kabla ya kushinda kuwa Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Arusha, Sabaya aliwahi kuwa mkuu wa wilaya kama ilivyokuja kuwa kwa mwanawe Lengai baadaye.

Jina la Lengai Ole Sabaya limeibua mjadala zaidi kutokana na historia yake; ana Shahada ya Sayansi katika Hisabati. Katika siasa amewahi kuwa diwani pekee wa CCM mwaka 2015 katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, kipindi hicho upinzani uliiangusha CCM. Zilikuwa enzi za "mafuriko ya Edward Lowassa".

Mwaka 2017, alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa wa Arusha na mwaka mmoja baadaye akateuliwa na Rais Magufuli kuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro.

Uteuzi huo ulifanya Ole Sabaya kuwa mkuu wa wilaya mdogo zaidi miongoni mwa walioteuliwa, akipangiwa kituo cha kazi cha Hai, eneo ambako ndiko jimbo lililokuwa chini ya uongozi wa Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe.

Ole Sabaya alianza kulalamikiwa hadharani na Mbowe mwaka 2019 kwa madai ya kuwarubuni wenyeviti 20 wa serikali za vijiji waliohamia CCM ghafla wakitokea CHADEMA.

Baada ya hapo, Ole Sabaya alianza kuandamwa na tuhuma mbalimbali, hasa za kundi la wafanyabiashara na baadhi ya watu waliodai anakandamiza upinzani ili kumdhibiti Mbowe.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Hai alipotangaza Mbowe kuangushwa katika kinyang'anyiro cha ubunge mwaka 2020, Mbowe na CHADEMA walimlalamikia hadharani Ole Sabaya wakieleza kupanga matokeo kabla ya kura kupigwa.

Ole Sabaya pia alifanya matukio mbalimbali yaliyoibua hisia za kitaifa, ikiwamo kukamata fedha bandia Sh. milioni 800 pamoja na tukio na kuvunja kampuni ya upatu ya Qnet iliyolalamikiwa kutapeli walimu na wastaafu.

Mei 13, 2021, Rais Samia alimsimamisha kazi Ole Sabaya kama mkuu wa wilaya kupisha uchunguzi na tarehe 4 mwezi Juni mwaka huo alifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha kujibu mashtaka mbalimbali.

Tarehe 15 mwezi Oktoba mwaka 2021, Ole Sabaya alihukumiwa kifungo cha miaka 30 gerezani kwa kosa la unyang'anyi wa kutumia nguvu, kwa kosa la kuiba fedha taslimu 390,000 toka kwa Diwani wa Sombeni, Bakari Msangi.

Miezi saba baadaye, Mahakama Kuu ilifutilia mbali hukumu hiyo kwa kile ilichokieleza kwamba ushahidi wa mashahidi ulipishana sana kuhusu kiini cha tukio.

Mwezi mmoja baadaye Sabaya alishinda kesi nyingine ya uhujumu uchumi mbele ya Hakimu Mfawidhi Patricia Kisinda iliyofunguliwa wakati anakamatwa.

Sabaya alihamishiwa Moshi kukabiliana na mashtaka mengine ambayo baadaye yaliondolewa mahakamani.

Tarehe 5 mwezi wa nne mwaka 2023 baada ya kukaa jela kwa siku 672, Ole Sabaya aliachiwa huru na toka wakati huo ameonekana hadharani mara moja mnamo tarehe terehe 4, 2024 katika Kanisa la Ebeneza Restoration, akimshukuru Mungu.

Katika mjadala wa warithi wa Makonda CCM, Ole Sabaya anatajwa kama kijana mwenye uwezo mkubwa wa kujenga hoja, kusimamia anachokiamini na kutokuwa na sifa ya ndumila kuwili, tabia ambayo wanasiasa wengi wanatajwa kuwa nayo.

Kuna wanaokwenda mbali zaidi na kudai kuwa kikao cha Kamati Kuu na Halmashauri Kuu ya CCM kitakutana Aprili 4, mwaka huu, kwa ajili ya kujaza nafasi zilizoachwa wazi na walioteuliwa kwenda kwenye majukumu serikalini.

Inadaiwa kuwa kwa sasa Rais Samia anasuka safu ya kumsaidia na kukisaidia chama kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Oktoba mwaka huu na Uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka 2025, ikiwa ni uchaguzi wake wa kwanza akiwa Rais.

Wakati Polepole ndiye Katibu Mwenezi aliyempokea Rais Samia ambaye baadaye akawa Mwenyekiti wa CCM Aprili, 2021, baadhi ya watangulizi wa nafasi hiyo kihistoria ni: Kingunge Ngombale-Mwiru, Omari Ramadhani Mapuri, John Mgesa, Jackson Msome, John Chiligati,

## HABARI KITAIFA

# Chanzo kukatika kwa umeme nchini chatajwa

**Na Halfani Chusi**

NAIBU Waziri Mkuu, Dotto Biteko ameeleza chanzo cha kukatika kwa umeme kwa mikoa iliyoungwa kwenye gridi ya taifa kwa zaidi ya saa 12 ni maji kuingia kwenye mitambo ya kufua umeme Kidatu, mkoani Mororgoro na kusababisha ijizime.

Biteko ambaye pia ni Waziri wa Nishati, alifanya ziara jana mchana baada ya kukosekana umeme usiku wa kuamkia jana na kujionea kazi iliyokuwa inafanywa na mafundi ili kurejesha nishati hiyo.

"TANESCO wamechukua hatua tangu jana usiku kwa kuyaondoa maji yaliyosababishwa na mvua nyingi kupita kiasi, wamefanyakazi usiku kucha kwa sababu yameingia kwenye mitambo yakachanganyika na mafuta," alisema na kuongeza:

"Ilibidi kufungua mitambo na kusafisha na kuweka 'oil' safi, tunafurahi wamefanyakazi kubwa na hivi tunavyozungumza (jana jioni) umeme umerejea sehemu kubwa ya nchi na kuna matengenezo yanaendelea ili kurudi kwenye hali ya kawaida," alisema.

"Ninawatoa hofu Watanzania, hii ni kutokana na mvua kubwa iliyonyesha maeneo mengi, wafanyakazi wa TANESCO wamesafiri usiku, tumesitisha mapumziko na kuhakikisha kazi inafanyika.

"TANESCO wanafanya kila linalowezekana ili kila mteja wetu apate huduma, ninawapa pole kwa shida walioyoipata usiku hadi leo jioni," alisema.

"Hawa mafundi hawajalala, wamefanyakazi ya kutoa maji kwenye mitambo, kwa niaba ya Watanzania nawapongeza sana. Mkurugenzi wa TANESCO hajakaa ofisini na kupiga simu bali amesafiri usiku kucha kuhakikisha kazi inakamilika.

"Furaha yetu ni watu kuwa na umeme, kama hawana umeme hatuna furaha, huu ndio mwendo wa TANESCO kutatua changamoto za watu kwa haraka. Asilimia 43 ya matatizo ya kukatika kwa umeme kwa sasa ni mvua, nguzo kuanguka na sio mgawo, kama hakuna timu (wafanyakazi) ya kutatua shida kwa haraka watu wataamini mgawo bado upo.

"Hatuna upungufu wa umeme, mgawo umepungua kwa kiasi kikubwa sana, kwa kipindi cha wiki moja hatuna mgawo kabisa kama hakuna umeme basi ni changamoto zilizopo za miundombinu."

Kwa mujibu wa Biteko, mvua ya mwaka huu imesababisha madhara kwenye maeneo mbalimbali na kwa sekta ya umeme kuna nguzo na miundombinu mingine kuharibiwa.

Aidha, alisema wamechukua tahadhari ili kupunguza madhara yanayoweza kusababishwa na ongezeko la mvua, huku akitoa mfano maji yaliyojaa kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo limejaa kabla ya makadirio ya mwaka 2026.

Alisema uwezo wa kushikilia maji ni mdogo, wataanza kuyafungulia na kwamba wamezima mtambo namba tisa kwa muda ili kuruhusu yatoke.

Vile vile, hatua za awali ni kuunganisha na kituo cha Pangani ili kuwasha mtambo wa gesi ambao umeendelea kusambaza umeme Dar es Salaam na Pwani.

Mapema jana mchana, Nipashe iliongea na msemaji wa TANESCO, Kenneth Boymanda na kusema changamoto hiyo ilitokea jana majira ya saa 8:22 usiku na kusababisha mikoa inayounganishwa na gridi hiyo kukosa umeme.

Alisema sababu ni hitilafu iliyotokea katika mfumo wa kudhibiti kiwango cha maji kwenye mitambo ya kufua umeme Kidatu, na kushindwa kuzuia mtiririko mkubwa wa maji yanayoingia kwenye mitambo hali iliyosababisha kujizima ghafla ili kujilinda.

Alisema mikoa iliyoathirika ni pamoja na Dar es Salaam, Tanga, Unguja, Pemba na Pwani huku akisisitiza juhudi za kuurejesha maeneo mengine zinaendelea.

"Katika mikoa mingine umeme unaendelea kurejea na jitihada za kufikia maeneo yote tunaamini mpaka kufikia leo (jana) mchana umeme utakuwa unapatikana nchi nzima.

"Tatizo hilo huwa linatokea mara chache sana na ndio maana limekuwa na athari kubwa, lakini tunaangalia namna ya kufanya lisiweze kutokea tena," alisema Boymanda.

Huko Zanzibar, Shirika la Umeme (ZECO) kupitia taarifa yake kwa umma limesema kukatika umeme katika eneo lote la Kisiwa cha Unguja kumetokana na hitilafu katika laini ya kusafirishia umeme iliyoko Tegeta mkoani Dar es Salaam.

Sehemu ya taarifa hiyo ilisema kumetokea changamoto ya kukatika kwa umeme tangu jana majira ya saa 8:30 usiku na kwamba hiyo ni taarifa ya awali na shirika linasubiri zaidi ufafanuzi kutoka kutoka Tanesco.

Februari 25, mwaka huu, Naibu Waziri Mkuu, aliwasha mtambo namba tisa katika Bwawa la Mwalimu Nyerere na kuingiza Megawatt 235 kwenye gridi ya Taifa, na kupunguza mgawo kwa asilimia 85.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri Mkuu Biteko, upungufu uliokuwapo ni megawatt 200 hadi 400, hivyo kuwashwa kwa mtambo namba tisa kumefanya nchi kuwa na umeme wa ziada megawatt 70, hata kabla ya kuwasha mitambo mingine minane iliyo katika ujenzi.

Mradi huo wenye thamani ya Sh. trilioni 6.6, ulianza kutekelezwa mwaka 2015 na ukikamilika yazalisha megawatt 2,115.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MBINGA**
**MBINGA**
**SHAURI LA KAZI HUKUMU NO. 2886/2024**
**KATI YA**
**AMSEK SECURITY SERVICE LTD...**
**MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**CHINA HENAN INTERNATIONAL COOPERATION GROUP C.O.LTD (CHICO)...MJIBU MAOMBI**

**KWA: CHINA HENAN INTERNATIONAL COOPERATION GROUP C.O.LTD (CHICO)**

**WITO**

Unaamuriwa kufika Mahakamani tarehe 08/04/2024 saa mbili na nusu asubuhi siku ambayo shauri tajwa hapo juu limepangwa kwaajili ya kutajwa.
Imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 20/03/2024

L.B MWAPEMELA
HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI
MAHAKAMA YA WILAYA MBINGA

NMB
Karibu yako

**TAARIFA KWA UMMA**

Mpendwa Mteja,

Tunapenda kukutaarifu kuhusu ada mpya za huduma zetu zifuatazo kuanzia **tarehe 2 Mei, 2024.**

| Aina ya Ada | Ada (TZS) |
|---|---|
| Kutoa Pesa katika ATM nje ya Tanzania | TZS 10,030 + 1% ya kiwango unachotoa |
| Miamala ya POS (Point Of Sale) za kimataifa na Manunuzi ya Mtandaoni | 1% ya kiwango cha muamala |
| Kupata Kadi ya ATM ya Standard/Tanzanite | TZS 11,800 |
| Kutoa Pesa katika ATM (UBX) | Kiasi (TZS) 1,000 - 199,999: 2,000; 200,000 - 400,000: 2,200 |
| Ada ya mwaka - Kadi ya World Debit | TZS 150,000 |
| Kutuma Pesa NMB kwenda NMB (ATM na Matawi) | see below |

Kutoa Pesa katika ATM (UBX)

| Kiasi (TZS) | Ada (TZS) |
|---|---|
| 1,000 - 199,999 | 2,000 |
| 200,000 - 400,000 | 2,200 |

Kutuma Pesa NMB kwenda NMB (ATM na Matawi)

| Kiasi (TZS) | Ada (TZS) |
|---|---|
| 0 - 9,999 | 50 |
| 10,000 - 29,999 | 100 |
| 30,000 - 99,999 | 450 |
| 100,000 - 499,999 | 1000 |
| ≥500,000 | 1300 |

Kwa taarifa zaidi, tafadhali piga **0800 002 002** au tutumie barua pepe kupitia: **tuambie@nmbbank.co.tz**

**Imetolewa na Utawala wa NMB Bank Plc.**

www.nmbbank.co.tz

# Askofu ataka wananchi kuombea uchaguzi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

ASKOFU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kati, Mchungaji Dk. Syprian Hilinti, amewataka wananchi kushiriki kuombea uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu, lakini wasichague viongozi wa dhuluma, majambazi na wala rushwa.

Akizungumza juzi wakati wa ibada ya Pasaka, kwenye Kanisa la KKKT Usharika wa Emmanuel, alisema waamini wa kanisa hilo waombee uchaguzi na wenye sifa waingie kwenye kinyang'anyiro kugombea nafasi mbalimbali kwa kuwa maombi ni kampeni kubwa na Yesu ni ujumbe wa maisha.

"Mwaka huu tuna uchaguzi wa serikali za mitaa, 2025 uchaguzi mkuu, chagua haki na kweli, usichague mtu wa dhuluma, jambazi, mla rushwa hata akiwa ndugu yako, ukoo wako, kabila lako, wa chama chako au wa dini yako, kama hafai usimchague," alisema.

Askofu Dk. Hilinti alisema Yesu Kristo alikuwa wa haki na waamini wafuate haki na kweli kwa kuchagua viongozi sahihi watakaoleta maendeleo nchini.

Akizungumza kuhusu tatizo la umeme, alimshukru Naibu Waziri Mkuu ambaye pia ni Waziri wa Nishati, Dotto Biteko, kwa kuendesha timua timua ya watendaji wazembe ndani ya Shirika la Ugavi Umeme (TANESCO) hali ambayo imeleta ahueni ya upatikanaji wa umeme nchini.

"Umeme unahitajika kimwili na hata kiroho, namshukru sana Naibu Waziri Mkuu, Dk. Biteko kutimua timua pale kwenye Tanesco," alisema.

Aidha, Askofu Dk. Hilinti alimshukru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu wanaotaka kufanya maandamano na kwamba hilo ni somo kwa watawala wengine wafuate haki na kweli.

"Sijaona Rais kama huyu (Samia) anaruhusu watu waandamane hapa sisi kama viongozi wa dini tunasema haki huinua taifa, tunapomsifu huyu mama hatuna maslahi binafsi na yeye wala ninapomsifu Dk. Biteko hatuna maslahi binafsi," alisema.

Alisema viongozi wa dini panapotakiwa kusifia viongozi watafanya hivyo na panapohitaji kukosolewa watakosoa na wala hawaogopi kufanya hivyo.




Mkuu wa Kitengo cha Udhibiti wa BancABC Tanzania (kulia) akimkabidhi msaada wa vyakula mbali mbali Mkurugenzi wa Kituo cha Watoto yatima cha New Faraja, Zamda Idrisa kilichopo Mburahati Jijini Dar es Salaam. BancABC Tanzania ambayo ni kampuni tanzu ya Atlas Mara ilitoa msaada wa vyakula mbalimbali pamoja na kuandaa futari kwa watoto waliopo kwenye kituo hicho kama ishara ya kuonyesha upendo kwenye kipindi hiki cha Mwezi Mtukufu wa Ramadan. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Viongozi wa majeshi watembelea TCRA kujifunza usalama mtandaoni

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa chuo cha maofisa wakuu wa Jeshi la Uganda (SCSC), ukiongozwa na Meja Jenerali, George Igumba, umetembelea Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kwa lengo la kujifunza masuala ya usalama mtandaoni.

Maofisa hao ni sehemu ya viongozi wa majeshi ya ulinzi katika nchi za Afrika Mashariki, ambao wanaongeza maarifa na ujuzi kuhusu usalama wa mtandao na TEHAMA.

Ujumbe huo uliojumuisha maofisa wakuu wa mafunzo na wanafunzi wa chuo hicho ulijumuisha maofisa wa ngazi za juu kutoka nchi mbalimbali kama Kiongozi wa Taasisi ya Mafunzo ya kijeshi ya India, Brigedia Jenerali Bhupendra Singh Fogat.

Wengine ni wanajeshi kutoka Kenya, Rwanda, India, Uganda, Sudan Kusini, Burundi, Afrika Kusini na Malawi, mpango ambao uliwezeshwa kwa mwaliko wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania chini ya uratibu wa Kanali Robert John Mbuba.

Walipowasili makao makuu ya TCRA jijini Dar es Salaam, ujumbe huo wa kijeshi ulipokewa na Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari ambaye aliwatembeza katika makumbusho ya mawasiliano na kufanya mawasilisho ya shughuli za mamlaka hiyo na sekta ya mawasiliano, ulinzi wa anga la mtandao na majukumu ya mamlaka za usimamizi.

Akizungumza baada ya kujifunza, Meja Jenerali George Igumba aliishukuru TCRA kwa fursa ya kuelewa kwa kina masuala muhimu ya usimamizi wa mawasiliano.

"Tunashukuru sana kwa TCRA kutupatia fursa hii ya kujifunza, na tunaamini wanafunzi wetu wamepata ufahamu muhimu wa sekta ya mawasiliano," alisema.

Aidha, alisisitiza umuhimu wa kubadilishana uzoefu, ujuzi na kujenga uwezo wa wanajeshi katika enzi ya maendeleo ya haraka ya teknolojia hususani katika teknolojia ya habari na mawasiliano.

Maofisa hao pia walishuhudia mabadiliko ya teknolojia ya mawasiliano kupitia makumbusho ya mawasiliano yanayosimamiwa na TCRA.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma TCRA, Rolf Kibaja, alisisitiza umuhimu wa makumbusho kuwa ni rasilimali ya elimu ya kipekee inayohifadhiwa na TCRA.

Mbali na ziara ya maofisa wa kijeshi, Kibaja aliwakaribisha na kuwahimiza wadau mbalimbali, ikiwamo wanafunzi kutembelea makumbusho ya mawasiliano.

"Kuingia katika makumbusho ni bure, tumejizatiti kuhakikisha watu wengi zaidi wanapata ufahamu wa teknolojia za mawasiliano, hivyo wadau wote hasa wanafunzi wanakaribishwa katika makumbusho yetu ya mawasiliano kwa ajili ya kujifunza," alisisitiza.

Ziara ya mafunzo, iliyoandaliwa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na kuongozwa na Kanali Mbuba, ni ya ushirikiano iliyolenga kukuza, kubadilishana maarifa na kuimarisha uwezo wa kiteknolojia wa vikosi vya kijeshi.

Hatua hii inalenga kuimarisha ushirikiano kati ya mataifa yanayoshiriki na kurahisisha kubadilishana uzoefu na ujuzi katika tasnia ya ulinzi.

## Watoto kituo cha New Faraja wafuturishwa, wapata msaada wa vyakula

**Na Mwandishi Wetu**

WATOTO wanaolelewa na kituo cha watoto yatima cha New Faraja Mburahati, jijini Dar es Salaam wamepewa msaada vyakula na kuandaliwa futari ikiwa ni ishara ya kuonyesha upendo kwenye kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadani.

Akizungumza jijini Dar es Salaam baada ya kukabidhi msaada huo, Mkuu wa Idara ya Udhibiti BancABC Tanzania, Saleh Geva, alisema benki hiyo imetoa msaada pamoja na kufuturisha watoto wa kituo hicho kama ishara ya kuonyesha upendo pamoja na kuwapa tabasamu.

"Watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu wanahitaji kuonyesha upendo. Sisi BancABC Tanzania na hasa wafanyakazi tumefarajika sana kujumuika nao pamoja na kupata wasaa wa kufuturu na watoto wanaolelewa kwenye kituo hiki.

"Kilikuwa ni kipindi faraja sana kwao, lakini furaha kwetu kuona watoto hawa wakitabasamu. Lengo letu ilikuwa ni kufanikiwa kuona watoto hawa wanajisikia kama sehemu ya jamii ya Watanzania," alisema Geva.

"Kuwafanya watoto hawa watabasamu na kufurahi kunawapa matumaini yao ya maisha ya baadaye. Kuja kwetu kufuturu na watoto hawa kumetuonyesha kwanini BancABC Tanzania imekuwa ikijikita sana kwenye kusaidia jamii inayotuzunguka. Tutaendelea na utamanduni huu wa kusaidia jamii inayoishi kwenye mazingira magumu kwa sababu tunaamini ni moja kati ya nguzo ya sisi kuendelea kukua kibiashara," alisema.

"BancABC Tanzania, ikiwa ni taasisi ya kutoa huduma za kifedha imekuwa ikifanya kazi kubwa kuwafikia Watanzania na hasa wale ambao bado hawajafikiwa na huduma za kibenki. Kwa sasa, BancABC Tanzania tunao mawakala zaidi ya 700 nchini kote," alisema Geva na kwamba benki hiyo inayo akaunti maalum kwa ajili ya wajasiriamali wadogo na wa kati kwa ajili ya kutoa mikopo ya kuimarisha biashara zao.

Mkurugenzi wa Kituo cha New Faraja, Zamda Idrisa alisema wamefarijika kwa kuona taasisi binafsi ikiunga mkono jamii ambayo inaishi kwenye mazingira mangumu.

"Msaada wenu umekuja kwenye muda mwafaka kwani watoto hawa wanahitaji kuonyeshwa upendo kama watoto wengine. Tunawashukuru kwa msaada wenu na tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kuwafungulia riziki kwenye maisha yenu ya kila siku," alisema.




Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Al-hikma Foundation, Nurdin Kishik, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu kuwasaidia waislamu 100, wasio oa wala kuolewa wanaotaka kufunga ndoa ambapo taasisi hiyo itagharamia (kushoto) ni Katibu wa Taasisi, Salum Kiza, na kulia ni Makamu Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Answar Hussein. PICHA: JUMANNE JUMA

# Mauaji ya watu yarindima Pasaka

**Na Waandishi Wetu**

MATUKIO ya mauaji yameripotiwa katika baadhi ya mikoa nchini wakati wa sikukuu ya Pasaka licha ya viongozi wa dini kukemea ukatili huo.

Mkoani Mara, mkazi wa kijiji cha Keroti, wilayani Tarime, Marwa Menganyi, anadaiwa kuua mtoto wake, Celina Marwa mwenye umri wa miezi minne kwa kumbana pumzi mdomoni na puani kisha kumdumbukiza kwenye jaba lenye maji hadi kufa.

Anadaiwa kutenda ukatili huo kwa lengo la kuchangiwa fedha za rambirambi kutoka kwenye vikundi vyake, ili imsaidie kumaliza madeni yanayomkabili kijijini huko.

Akisimulia tukio hilo mama wa marehemu, Bagheni Marwa alidai mumewe alitekeleza ukatili huo baada ya kuwa amekwenda kufua nguo za mtoto ambako alifuatwa na mtoto mwingine kumpatia taarifa hizo.

"Alikuja ananiambia njoo umwone mtoto amezama kwenye jaba na kweli nilipofika nyumbani nilimkuta kwenye jaba kichwa chini miguu juu," alidai mama huyo.

Aliendelea kueleza kuwa baada ya hapo alitoa taarifa kwa mwenyekiti wa kijiji ambaye alitoa taarifa polisi kuwa kuna kifo chenye utata katika eneo lake, akitaka wafike kuchunguza, lakini mume wake alikataa asichunguzwe na kusema waache, azikwe hivyohivyo, hakuna tatizo.

"Akakataa kabisa, mimi ninaona sababu ni madeni ya vikundi maana vilikuwa vinapishana tu kuja kudai fedha zao, hivyo akaamua kufanya ukatili huo, ili achangiwe rambirambi kutoka kwenye vikundi vyake ili imsaidie kumaliza madeni hayo.

"Kila mara alikuwa anadai kutaka kujinyonga, lakini mama yake akamshauri asifanye hivyo, bali atafute njia nyingine ya kupata fedha kulipa alikokuwa akidaiwa," alidai Wagesa Magheni, mama mdogo wa marehemu.

Mama wa mtuhumiwa huyo, Ester Ntono alieleza kusikitishwa na tukio hilo huku akikana kuhusika katika mipango ya kuuawa mjukuu wake na kutaka watu waache kumsingizia na kumhusisha katika mipango isiyomhusu.

Jirani wa familia hiyo, Ghati Matiku alidai kuwa baada ya kufika eneo la tukio, walibaini mtoto alitumbukia kwenye maji, lakini cha kushangaza hakuwa amekunywa maji hayo, hali iliyozua utata.

Nyangi Kinga, mmoja wa wanavikundi alikokuwa akidaiwa fedha, alidai mchakato wa kumpa fedha za rambirambi ulikuwa tayari umekamilika, lakini baada ya kupata taarifa hizo ilibidi wasitishe na pia kuendelea kumdai deni lao la awali.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Nyabigena, Muhere Mang'era alisema kuwa baada ya kubaini utata huo, aliita polisi ambao walifika na kuanza uchunguzi kwa kuhoji mama, baba, majirani na uongozi wa kijiji ili kupata taarifa kamili.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Tarime/Rorya, Marck Njera alithibitisha kuwa mwili wa marehemu ulipofanyiwa vipimo, ilibainika kifo chake kimesababishwa na kuzibwa mdomo na pua na kukosa pumzi, si maji ya jaba.

Alisema tayari jeshi hilo limemkamata baba wa marehemu ambaye alidaiwa kuhusika na ukatili huo alipoachiwa mtoto huyo nyumbani kwake na kuwa jeshi hilo linaendelea na uchunguzi. Baada ya kukamilika, hatua nyingine za kisheria zitafuata.

**MWANASHERIA AUAWA**

Mkoani Dar es Salaam, Alex Mazengero, anayedaiwa kuwa ni mwansheria, ameuawa kwa kucharangwa mapanga na watu wasiojulikana alipokwenda kwenye eneo la mteja wake lenye mgogoro.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mtoni Mtongani, wilayani Kinondoni, Stanslaus Mnyonge, alisema Mazengero alikuwa mkazi wa mtaa huo kwa kipindi cha nyuma na alikuwa anafuatilia mgogoro huo kwa muda mrefu.

Alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa moja usiku katika eneo la Tegeta Skanska ambako mwanasheria huyo alikuwa akikimbilia kujiokoa, lakini hakupata msaada.

Akielezea tukio hilo, mwenyekiti huyo alisema kijana huyo alikwenda kwenye eneo hilo la ardhi kuangalia eneo la mteja wake ndipo wakajitokeza vijana wanne ambao walimkata kwa panga kichwani.

Alisema mwanasheria huyo alianza kukimbia ili kujiokoa, lakini waliendelea kumkimbiza hadi eneo la Skanska, ndipo alianguka chini na walifika wakamkata zaidi hadi umauti ulipomfika.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alithibitisha kuwapo mgogoro wa ardhi na mauaji hayo.

"Ni kweli kuna mtu mmoja ameuawa kwenye mgogoro wa ardhi, hapa nilipo sina taarifa za kina ila tukio kama hilo lipo," alisema Kamanda Muliro.

Mmoja wa madereva daladala, alisema "marehemu alikuwa anavuja damu maeneo ya kichwani na maeneo ya mikononi kwa wingi sana."

Alisema inasikitisha kuona watu walishindwa kumsaidia kutokana na kwamba watahamishiwa kuhusika na mauaji.

**MWALIMU, MWANAFUNZI**

Mkoani Mbeya, watu wasiojulikana wamevamia nyumba moja wilayani Chunya na kuua mwalimu wa shule ya msingi na mwanafunzi wa shule ya sekondari na kujeruhi mtoto kisha kutokomea kusikojulikana.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi Benjamin Kuzaga alitaja waliouawa kuwa ni Heriety Lupembe (37) ambaye ni Mwalimu wa Shule ya Msingi Mbugani na Ivon Tatizo (15) ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Isenyela, wilayani humo.

Alitaja mtoto aliyejeruhiwa ni Haris Mtweve (6) ambaye pia ni mwanafunzi katika Shule ya Msingi Ken Gold ya wilayani humo.

Kamanda Kuzaga alisema tukio hilo lilitokea Machi 31, 2024 saa 2:30 usiku wakati watatu hao wakiwa sebuleni nyumbani kwao katika Kijiji cha Kiwanja.

Alisema uchunguzi wa awali ulibaini kuwa wahalifu hao waliwavamia watatu hao na kuanza kuwashambulia na baada ya kufanya hivyo walifunga milango kwa nje na kuondoka na funguo.

"Chanzo cha tukio hili hakijafahamika, lakini tunaendelea na uchunguzi, majeruhi ambaye ni mtoto Haris Mtweve anaendelea na matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya na afya yake haijaimarika," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema jeshi hilo linaendelea kufanya msako ili kunasa wahusika wa tukio hilo na kuwachukulia hatua za kisheria, akiomba wananchi ambao wana taarifa zozote ambazo zinaweza kusaidia kunasa wahusika wazitoe kwa siri.

Alisema wahalifu hao wakikamatwa watachukuliwa hatua kali za kisheria kutokana na kosa hilo la jinai ambalo adhabu yake mahakamani ni kunyongwa hadi kufa kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16.

Baadhi ya wananchi wa kijiji hicho cha Kiwanja walisema walishtuka baada ya mwalimu huyo kutofungua duka lake na simu yake kutopatikana huku pia akiwa hajahudhuria kanisani, hali iliyowatia wasiwasi.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kiwanja alikokuwa anaishi mwalimu huyo, Gideon Kinyamagoha alisema walifika nyumbani kwa mwalimu huyo na walipoingia ndani kwa kuvunja mlango, walikuta sururu ikiwa na damu na marehemu wawili wakiwa wamelala chini na majeruhi ambaye ni mtoto akiwa kando.

Alisema walitoa taarifa polisi na askari walifika na kufanya uchunguzi wa awali kisha kuchukua miili na kwenda kuihifadhi Hospitali ya Wilaya ya Chunya na majeruhi alikimbizwa Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya.

Inadaiwa marehemu aliagiza bidhaa za dukani kutoka Mbeya na watu alioagiza baada ya kumkosa nyumbani kwake na hata kwenye simu waliziweka nje, wakiamini alikuwa ametoka na angezikuta baada ya kurejea.

***Imeandaliwa na Vitus Audax (MUSOMA), Salehe Mpili na Tuntule Swebe (DAR) na Nebart Msokwa (MBEYA)**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ujumbe wa viongozi wa dini utiliwe maanani

**WAKATI** wa maadhimisho ya Sikukuu ya Pasaka (kumbukumbu ya kufufuka kwa Yesu Kristo), viongozi mbalimbali wa madhehebu ya dini ya kikristo pamoja na viongozi wa kiserikali, walitoa ujumbe mzito kuhusu maadili ambao hauna budi kufanyiwa kazi ili kuepusha kuendelea kuona maadili hayo yakiporomoka siku hadi siku.

Mambo makuu yaliyozungumzwa na viongozi hao ni kuhusu vitendo vya rushwa kushamiri katika maeneo muhimu ambayo wananchi ni kimbilio lao na kutegemea kupata haki zao, ukatili dhidi ya watu wengine, ambao kwa miaka ya hivi karibuni kumeshuhudiwa vitendo vingi vya mauaji au kufanyiana vitendo vya kinyama na vile vile mapenzi ya jinsia moja kuingia kwa kasi.

Kushamiri kwa kuporomoka kwa maadili sio dalili nzuri hivyo kuna kila sababu viongozi wakiwamo wa dini kulizungumzia ili watu warudi kwenye imani zao na kumwogopa Mungu.

Vitendo vya rushwa vimekuwa vikikwamisha mambo mengi na wakati mwingine kusababisha dhuluma kwa watu wanaostahili kuwa na haki ya kumiliki mali au kupata haki.

Mauaji au vitendo vya kinyama baadhi chanzo chake kinatokana na rushwa.

Mtu anayestahiki kupata haki anadhulumiwa na kutokana na uonevu huo, aliyedhulumiwa anaamua kufanya jambo lolote ikiwamo kuua ili wote wakose.

Suala la maslahi duni pia linasababisha baadhi ya watumishi wa umma na wanaofanyakazi kwenye sekta binafsi kutumia mbinu nyingine ya kujiongezea kipato na matokeo yake kujiingiza kwenye vitendo vya rushwa na kuendelea kuota mizizi.

Rushwa ni tatizo kubwa kiasi cha kusababisha hata mtu anapopatiwa huduma anayostahili anaona kama amependelewa na kuamua kutoa pesa kuonyesha shukrani.

Mauaji katika jamii yanayosababishwa na wivu wa mapenzi, yameshamiri na hii inatokana na walio kwenye mahusiano kushindwa kuaminiana kutokana na kutomtanguliza Mungu mbele.

Hata watoto wasio na hatia wanaingizwa kwenye unyama huu kwa sababu tu wazazi wameshindwa kuelewana na wao kuwa waathirika.

Suala la mapenzi ya jinsia moja ni tishio kwa vijana wengi na hiyo inatokana na tamaa ya kuishi maisha wasiyokuwa na uwezo nayo na vilevile kuiga utamaduni wa nchi za kimagharibi.

Vijana wengi wanaangamia kwa sababu hawataki kufanyakazi, lakini wanataka kuishi maisha ya hali ya juu ya kuendesha magari mazuri na kuishi kwenye nyumba za kifahari na kuvaa mavazi ya gharama.

Wengi huishia kulelewa na wanawake watu wazima walio umri sawa na mama zao na wengine kutumbukia kwenye mapenzi ya jinsia moja.


Kijana wa kiume anaonekana ana nguvu za kutosha kufanyakazi na kupata kile anachokitaka, lakini hataki kufanyakazi na badala yake anaishia kujiremba kama mtoto wa kike kwa kuvaa hereni na kujichubua ngozi ili aonekane na mvuto.

Hali hiyo haithiri vijana wa kiume pekee, hata kwa vijana wa kike wapo wanaopendana na kuoana wenyewe kwa wenyewe.

Hii inafikirisha kwa kuwa kama vijana hao ndio tegemeo la taifa la baadaye halafu wanaachwa wakiangamia, tutakuwa na taifa la namna gani.

Kauli za viongozi wa dini ni lazima zifanyiwe kazi ili kuepusha vijana wengi kuendelea kuangamia. Wazazi wana jukumu kubwa la kufuatilia watoto wao nyendo zao badala ya kuwaachia jukumu hilo walimu au wasaidizi wa nyumbani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kamati, bodi zimalize kero ya uhaba wa vyoo shuleni

**UHABA** wa matundu ya vyoo ni kero inayoendelea kuzikumba shule za msingi na sekondari, licha ya jitihada ambazo zimekuwa zikifanyika kunusuru wanafunzi kutoka mazingira hayo hatarishi.

Kwa muda mrefu vyombo mbalimbali, hasa vya habari vimekuwa vikiripoti kuwapo kwa uhaba lakini pia na ubovu wa vyoo katika shule za msingi na sekondari.

Mfano, Februari mwaka huu, vyombo vya habari viliripoti uhaba wa matundu vya vyoo katika Shule ya Msingi Kahama, katika Manispaa ya Ilemela jijini Mwanza.

Inaelezwa, shule hiyo ina wanafunzi 1,963 na matundu 15 ya vyoo, na kwamba uhaba huo unasababisha wanafunzi 130 kutumia tundu moja la choo kwa siku.

Katika maeneo mengine ya nchi, inaelezwa kuwa baadhi ya shule zina uhaba huo unaosababisha wanafunzi kujisaidia vichakani au katika vyoo vya nyumba za jirani na shule.

Kwa ujumla zinatajwa shule nyingi zina tatizo, ambalo wakati mwingine ni hatari kwa afya za wanafunzi, pia usalama wao, hasa vyoo vyenye nyufa.

Katika mazingira hayo ya uhaba wa vyoo, baadhi ya wanafunzi wanaripotiwa kujisaidia choo kimoja na walimu wao, kitendo ambacho kimsingi hakiko sawa.

Nadhani ni hali inayoweza kurudisha nyuma juhudi za walimu kutoa taaluma, kwani ni vigumu kwa mtoto kujifunza katika mazingira hayo.

Ingekuwa vyema sasa kuwapo kampeni maalum ya kuhakikisha kila shule inakuwa na matundu ya kutosha, ili kuondoa adha kwa wanafunzi na walimu.

Tunaambiwa kuwa kampeni ya 'nyumba ni choo' imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuhamasisha wananchi kuwa na vyoo vya kisasa, ninadhani kampeni hiyo ingehamia shuleni.

Ikumbukwe tatizo la uhaba wa vyoo sasa limeota mizizi katika shule za msingi na sekondari, ni wazi hazina vyoo vinavyokidhi mahitaji ya wanafunzi.

Hivyo, ni vyema kampeni hiyo ingetua shuleni ili kamati na bodi za shule zihamasike na kuona umuhimu wa shule kuwa na vyoo vya kutosha na tena bora.

Shule hizo ni za umma, ambazo hakuna budi kuzihudumia kadri inavyowezekana, kuanzia chakula cha wanafunzi na hata ujenzi wa miundombinu, ikiwamo ujenzi wa vyoo na hata madarasa.

Kamati na bodi ndizo zinazopanga kuboresha shule kwa kushirikisha wananchi ili waweze kuzihudumia badala ya kujiweka pembeni na kudhani hawahusiki.

Sidhani kwamba ni kosa wananchi kuchimba mashimo ya vyoo, kufyatua matofali na kujenga na kwa ajili ya watoto wao.

Cha msingi ni kuimarishwa mfumo wa ushirikishaji wa wananchi kwa mambo ambayo yanawahusu, ili nao wawe na mchango.

Binafsi ninaamini kwamba ujenzi wa vyoo vya shule umo ndani ya uwezo wa umma si wa kutafuta au kusubiri wafadhili. Jambo la muhimu ni ushirikishaji.

Umma au jamii inapaswa kujishughulisha na tatizo la wanafunzi kukosa vyoo,kupitia kamati na bodi za shule, huku serikali ikitia msukumo.

Kamati na bodi za shule zikifanya sehemu yake ya kushirikisha na kuhamasisha wananchi, huku serikali nayo ikitia msukumo, tatizo la uhaba wa vyoo au shule kuwa na vyoo vibovu linaweza kuwa historia.

Ikumbukwe kuwa, majukumu ya kamati na bodi za shule ni pamoja na kuandaa mipango ya maendeleo ya shule, kuhakikisha shule inakuwa na miundombinu na vifaa kamili na bora.

Vilevile, ni kutafuta vyanzo vya fedha kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya shule, hivyo ukubwa wa tatizo la vyoo katika shule za msingi na sekondari linaweza kuisha iwapo kamati na bodi zitawajibika vizuri.

Hapa kinachohitajika ni ubunifu na weledi wa kutatua kero za uhaba zinazozikabili shule badala ya kusubiri fedha kutoka serikalini, huku wananchi wapo ambao ndio wenye shule.

Kamati na bodi zinaweza kubuni vyanzo vingine vya mapato, ili kuboresha miundombinu ya shule, lakini pia wakati mwingine inawezekana kutatua tatizo kwa kutumia rasilimali zinazopatikana katika mazingira husika kama miti, mchanga na mawe na rasilimali watu kumaliza tatizo hilo sugu.

Aidha, kamati na bodi zinaweza kutoa elimu kwa wanajamii ili itambue shule za umma ni mali yao, hivyo wazihudumie kadri inavyohitajika badala ya kuachia serikali jukumu hilo.

## Vibarua TASAF wadai kutolipwa ujira

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

VIBARUA wanaotekeleza miradi mbalimbali kwenye jamii kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wamedai kudhulumiwa ujira wa kazi ambazo walizifanya kupitia mpango wa kunusuru kaya maskini na kuwafanya kuishi maisha magumu.

Vibarua hao wametoa kilio chao kwa nyakati tofauti juzi katika mkutano wa hadhara wa Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita wa kusikiliza na kutatua kero za wananchi, uliofanyika katika Kijiji cha Mitonga, Kata ya Nyamilango.

Mkazi wa Kijiji cha Mitonga, Machibya Marco alisema, wana miezi mitano wamefanyakazi ya miradi mbalimbali kwenye jamii, lakini mpaka sasa hawajalipwa ujira wao na kila siku wanatakiwa kulipwa Sh. 10,000 na kuiomba serikali kuingilia kati malipo yao yapatikane na kutatua shida zao.

Chausiku Juma, alisema mwaka jana walifanyakazi miezi sita na kulipwa miezi mitatu pekee na kuanzia Novemba mwaka huo mpaka sasa wanadai ujira wao na walipofuatilia kujua hatua yake walilipwa ujira wa mwezi mmoja, hatua inayowafanya kukata tamaa ya kuendelea kufanyakazi hizo.

Mery Leonard, alisema wanufaika wanaopokea fedha kupitia simu ya mkononi na benki waliahidiwa kupewa fedha ya kutolewa ili kutokatwa wanazopewa, kitendo hicho bado hakijafanyika na wanaendelea kukatwa malipo yao ambayo hayakidhi mahitaji yao na kushindwa kukua kiuchumi.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa halmashauri hiyo, Morgan Mwita akijibu malalamiko hayo, alikiri vibarua hao kutolipwa ujira wao kwa kipindi kirefu ikiwamo wanufaika na wanadai tangu mwezi Desemba, mwaka jana. Malipo yote ya nyuma yalilipwa tangu mwezi Septamba, mwaka jana.

Alisema, wamekuwa wakilipa fedha za walengwa wa TASAF kadiri zinavyopatikana, na mwezi huu watahakikisha madai yote yanalipwa na wanaodai hawakuweza kupata malipo yao tangu mwaka jana walipofika ofisini ili malalamiko yao yashughulikiwe.

Kuhusu fedha za kutolea zinazopita kwenye simu na taasisi za kifedha yamekuwa yakitolewa na serikali na kutoa mfano kwa wanufaika wanaopokea kiasi cha Sh. 100,000 hupokea Sh. 105,000 kama kiasi cha kutoa.

Mkuu wa wilaya, Mboni Mhita alisema, mradi ya maendeleo yanayotekelezwa kwenye jamii kupitia TASAF isije ikawa kero kwa wananchi na badala yake walipwe ujira wao kwa wakati ili wanufaika na rasilimali hiyo na katika utekelezaji wa miradi hiyo ni kuinua na kupunguza wimbi la umaskini kwa wananchi.



Mkuu wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Zainabu Abdallah (kulia) akipata maelezo kutoka kwa Mkandarasi wa kampuni ya ujenzi ya Mwalow, Mubaraka Mwalongo (Kushoto) alipotembelea kukagua ujenzi wa mradi wa daraja jipya eneo la Kwamtiga kata ya Genge ambalo litafunguliwa wakati wa mbio za Mwenge wa Uhuru Aprili 15 mwaka huu. Wapili kulia ni Meneja wa Tarura wilaya ya Muheza John Kwagilwa na watatu kulia ni Msimamizi wa mradi huo kutoka Tarura, Lidya Msumari. **PICHA:STEVEN WILLIAM**

# Kampuni mbili zakwama kushikilia tani za petroli

**Na Grace Gurisha**

KAMPUNI mbili za kigeni, Numora Trading PTE Limited kutoka Singapore na Lamar Commodity Trading ya Dubai zimekwama mahakamani kuendelea kushikilia tani 20,685.61 za petroli zenye thamani ya Sh. bilioni 43 mali inayodaiwa kuwa ya kampuni ya Prestige Investment kutoka Burundi.

Katika uamuzi uliotolewa hivi karibuni, Mahakama ya Rufani imetupilia mbali notisi za rufaa zilizowasilishwa na kampuni hizo mbili dhidi ya uamuzi uliotolewa na Divisheni ya Biashara ya Mahakama Kuu kuhusu shehena hiyo ya mafuta yaliyokuwa yanasafirishwa kwenda katika Jamhuri ya Burundi.

Majaji Mary Levira, Zepharine Galeba na Mustapher Ismail, waliamua kwamba notisi za rufaa zilizowasilishwa dhidi ya uamuzi wa Mahakama Kuu zinatokana na amri ndogo ambayo hatima yake haimalizi au kuamua kwa ukamilifu shauri lililopo mahakamani.

"Kwa hiyo, tunakubali ombi hilo na kufuta notisi ya rufaa kwa gharama," Majaji hao walisema katika uamuzi wao wa hivi karibuni kuhusu Kampuni ya Numora Trading PTE Limited. Majaji hao pia walifikia uamuzi kama huo wa kuikataa notisi nyingine ya rufaa iliyowasilishwa na Lamar Commodity Trading katika kesi hiyo.

Aidha, majaji hao walikataa ombi lililowasilishwa na Numora Trading PTE Limited, kutaka kuzuia utekelezaji wa uamuzi wa Mahakama Kuu kuhusu kuachia shehena hiyo ya mafuta kwa sababu maombi hayo yalikuwa yameegemea kwenye notisi ya rufaa ambayo imekataliwa.

Katika uamuzi wao, majaji walibainisha kuwa mawakili wote wanakubaliana kuwa shauri la msingi bado linaendelea mahakamani, hivyo haki hairuhusu rufaa kuwasilishwa katika shauri ambalo halijafikia uamuzi wa mwisho na uliotolewa na Mahakama Kuu.

"Tuna maoni kuwa mwisho ambao una athari ya kuruhusu rufaa chini ya kifungu cha 5 (2) (d) cha Sheria ya Mamlaka ya Rufaa ni mwisho wa shauri na sio sehemu ya masuala yaliyomo ndani ya shauri husika," majaji hao walisema.

Mbele ya Mahakama Kuu, mwombaji alilalamikia mienendo ya kampuni za Lamar Commodity Trading DMCCC na Nomura Trading PTE Limited, zilizosababisha kuzuiliwa kwa shehena yao ya mafuta ya petroli waliyokuwa wameagizwa kutoka nje kwa lengo la kuyasafirisha kwenda Jamhuri ya Burundi.

Ilidaiwa kuwa shehena hiyo iliuzwa kwa kampuni ya Lake Oil Limited huku mwombaji akitimiza wajibu wake wa malipo chini ya hati ya dhamana ya malipo ambayo ilitolewa na Benki ya KCB Kenya Limited kwa ajili ya Kampuni ya Nomura Trading PTE Limited.

Mahakama ilikuwa na maswali kadhaa wakati shehena hiyo inasemekana kuuzwa kwa Kampuni ya Lake Oils Limited, inayodaiwa kuwa na madai kwenye mafuta hayo.

Kadhalika, Mahakama ilijiuliza kama kulikuwa na mpango wa kuchepusha shehena hiyo kwa Kampuni ya Lake Oils Limited au ulikuwa ni udanganyifu kati ya Lamar Commodity Trading DMCCC na Nomura Trading PTE Limited na Lake Oils Limited kama ilivyobainishwa na wakili wa mwombaji.


Katika mawasilisho yake, wakili wa mwombaji, alidai kuwa mnamo Julai 6 au 7, 2023, Benki ya KCB Kenya Limited ilipokea pesa za dola za Kimarekani milioni 15 kwa shehena ya mwisho.

"Kama inavyoweza kubainika, iwapo Julai 7, 2023 hali ilikuwa hivyo na tarehe hiyo hiyo shehena hiyo ilidaiwa kuuzwa kwa (Lake Oils Limited), ukweli huo unaonesha nini? Je, haipendekezi kwamba uuzaji huo unaonesha vitendo vya ulaghai ikiwa hilo litatokea kuwa kweli?" mahakama iliuliza.

Wakati wa kusikilizwa kwa shauri hilo, Kampuni ya Prestige iliwakilishwa na Wakili Seni Malimi, huku Mawakili Nuhu Mkumbukwa, Stephen Axwesso, Godwin Nyaisa na Gasper Nyika wakiwakilisha Numora Trading PTE Limited, Lamar Commodity Trading, KCB Bank Kenya Limited na Lake Oil Limited.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Wazee waliopigana vita ya pili ya dunia walilia matunzo

**Na Beatrice Shayo**

CHAMA cha Askari Wastaafu wa vita kuu ya pili ya dunia iliyotokea mwaka 1939 hadi 1945 wameiomba serikali iwakumbuke na kuwatunza wazee hao kutokana na kutokuwa na uwezo wa kujihudumia na kujikuta wanaishi katika mazingira magumu.

Hayo yalielezwa jana jijini Dar es Salaam na Mwenyekiti wa Chama cha Tanzania Legion and Clubs (TLC), Hamis Kwizombe, wakati wa uchaguzi wa viongozi unaofanyika kila baada ya miaka mitatu.

Kwizombe alisema chama hicho kinajumuisha watoto na wajukuu, changamoto kubwa wanayokabiliana nayo wazee hao ni serikali kutowatambua na kuwathamini kwa miaka 50 hadi 70.

Alisema anaiomba serikali kuwasimamia kuwatunza hao kwa kuwa ndio waliobaki na ni tunu ya taifa ambayo imewakutanisha na inayofanya watu wengi kukimbilia Tanzania kama kisiwa cha amani waliyoipigania wazee hao.

Mmoja wa Mashujaa hao, Muhando Shangazi (104), alisema waliitumikia nchi bila kinyongo na sasa wameishiwa nguvu ni vyema wakakumbukwa na chochote ili wajikimu.

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Sixtus Mapunda, ameikataka chama hicho kutunza historia ya wazee hao kwakuwa ni muhimu katika historia ya nchi ambayo vijana wengi hawaifahamu.

Alisema wazee 52 walio hai hadi sasa kati ya 15,000 walioshiriki vita ya pili ya dunia ni hazina kwa taifa na wenye historia na nchi.

"Tumeambiwa kuwa kwenye vita ya pili ya dunia mwaka 1939 hadi 1945 ambayo sisi wote hapa tulikuwa hatujazaliwa walioenda vitani ni watu 15,000 waliorudi ni takribani 13,000 na hadi sasa walio hai ni 52 na mdogo zaidi ana miaka 100 hivyo ni muhimu kuwaandikia historia kabla hawajafa," alisema Mapunda.

Aidha, alitoa wito kwa waandishi wa habari kuwatafuta wazee hao waliopigana vita ya pili ya dunia na kutengeneza makala ambazo zitawezesha kuweka historia nzuri hususani ya picha ambayo itawasaidia vijana na kizazi kijacho kujua historia ya nchi yao.

Katibu Mkuu wa Chama hicho, Charles Lubara, alisema malengo ya chama ni kuhifadhi historia ya wazee kwa faida ya kizazi kilichopo na kijacho.

Alisema tayari wamewasiliana na Wizara ya Maliasili, wamepewa eneo mkoani Dodoma ambalo watajenga makumbusho itakayotumiwa na watu mbalimbali kwenda kujifunza historia ya nchi yao.




Wadau mbalimbali pamoja na wafanyakazi wa kampuni ya mafuta ya Puma Tanzania wakipata futari iliyoandaliwa na kampuni hiyo kwa ajili ya kufuturisha katika kipindi hiki cha mfungo wa Ramadhan jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# MOI yaja na mbinu mpya kwa wagonjwa

**Na Joseph Mwendapole**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), imeanzisha utaratibu wa kuwajulia hali wagonjwa kwa kuwapigia simu na ndugu zao ili kujua maendeleo yao na kupata maoni kuhusu hali ya utoaji wa huduma kwa taasisi hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Prof. Abel Makubi, aliongoza zoezi hilo mwishoni mwa wiki kwa kuwapigia baadhi ya wagonjwa na kuwajulia hali zao, kupata maoni yao na ushauri ili kuboresha huduma.

"Tumeamua kuwapigia simu wagonjwa wetu kuwajulia maendeleo yao na kuwapa fursa ya kutoa mrejesho juu ya hali ya huduma zetu ili tuweze kuboresha zaidi," alisema Prof. Makubi na kuongeza "Huu ni utekelezaji wa maelekezo ya Wizara ya Afya kutaka watoa huduma kuboresha mawasiliano na wateja wao na menejimenti ya MOI imeamua kuja na mbinu hii ambayo inatuwezesha kumfikia mgonjwa mmoja mmoja, kujua maendeleo na kupata maoni yake," alisema.

Pia, MOI imekuwa ikipata mrejesho kupitia kusikiliza maoni ya wagonjwa na watu wengine moja kwa moja na kupitia makundi ya WhatsApp, mikutano ya kila wiki katika banda la wagonjwa, sanduku la maoni, kupigiwa simu na ujumbe mfupi wa simu.

Profesa Makubi alisema maoni hayo yamesaidia menejimenti kujitathmini na kuboresha huduma kwa wateja wa taasisi hiyo.

Mwishoni mwa wiki MOI ilitoa zawadi ya Sikukuu ya Pasaka kwa watumishi wake 1,046, ili kuwapa motisha ya kufanya kazi kwa bidii na kutoa huduma bora kwa wagonjwa.

Zawadi hizo ambazo ni ilo 15 za mchele, lita mbili za mafuta ya kupikia na vinywaji zenye thamani ya shilingi 50,000 kwa kila mmoja na zimekabidhiwa kwa wawakilishi wa watumishi hao na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya MOI Prof. Abel Makubi.

Akizungumzia zawadi hizo, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali watu wa MOI, Orest Mushi, alisema menejimenti ya MOI imeamua kuwapa motisha watumishi wake ya mkono wa sikukuu za Pasaka na Eid El fitri ili waweze kusherehekea kwa furaha na pia kutambua mchango wao mkubwa wa kutoa huduma kwa wananchi wote.

Alisema zawadi hiyo ilitolewa kwa niaba ya wagonjwa na ni shukrani kwa watumishi kufanyakazi kwa moyo wa kujitolea, huruma, upendo na uwajibikaji wa hali ya juu.

"Ni imani ya menejimenti ya MOI kuwa tunaporudi baada ya Sikukuu za Pasaka na Eid, tutaongeza umahiri na uwajibikaji zaidi na kutoa huduma bora kwa wananchi," alisema Mushi.

Mmoja wa wafanyakazi wa MOI, Juma Rehani, aliishukuru menejimenti ya MOI kwa motisha hiyo na imewaongezea ari ya kufanya kazi.

"Naishukuru menejimenti kwa zawadi hii, tumefarijika sana na naahidi kwa niaba ya watumushi wenzangu kuwa tutafaendelea kutoa huduma bora kwa wagonjwa wetu," alisema Rehani ambaye ni muuguzi kiongozi huduma za upasuaji," alisema.

## Ziwa Tanganyika kufungwa kwa miezi mitatu

**Na Zatifa Ramadhani,** SAUT

SHUGHULI za Uvuvi katika Ziwa Tanganyika mkoani Kigoma zinatarajiwa kufungwa kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia mwezi Mei 15 hadi Agosti 15, mwaka huu lengo likiwa ni kupumzisha ziwa hilo kupata ongezeko la samaki.

Hatua hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kukuza sekta ya Uvuvi nchini kwa kusaidia ongezeko la samaki ziwani humo.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Kigoma, Salimu Kali wakati akizungumza na wadau, viongozi na wavuvi wanaotumia ziwa hilo na kutaja hatua hiyo kuwa pia sehemu ya kuongeza soko siku za usoni kutokana na uwapo wa samaki wa kutosha na wakubwa.

Kali alisisitiza umuhimu wa shuguli hiyo katika Ziwa Tanganyika na kusema kuwa kitovu cha mazao ya samaki hutokana na mazalia kuwa mengi na kukidhi mahitaji ya watumiaji.

"Sio tu kulipumzisha Ziwa Tanganyika, utafiti pia ulifanyika kwa nchi zote nne zinazotumia ziwa hili ikiwamo Tanzania, Kongo, Zambia na Burundi hivyo zilishirikiana na wakafikia makubaliano ya kulipumzisha kwa muda wa miezi mitatu kwa kila mwaka," alisema Kali.

Alisema walishirikisha viongozi wote wanaozunguka Ziwa Tanganyika kuanzia ngazi ya mtaa, wataalamu wa kuvua samaki pamoja na wazawa wa Kigoma na walitafuta muda ambao samaki wanapungua au kuisha kabisa ndio wakachagua miezi hiyo.

Katika hatua nyingine Kali alisema, wizara imekuja na suluhisho la kutengeneza vizimba kwa ajili ya ufugaji wa samaki pamoja na mbinu za kuwalisha samaki hao hivyo itasaidia pato la kila mmoja hususani kwa wategemezi wa shuguli ya uvuvi kwa ajili ya kujipatia kipato na pia itachangia pato la taifa.

"Tayari vizimba vimeshatengenezwa na mwezi Aprili vinatarajiwa kugawiwa kwa wavuvi kama utaratibu uliotumika kugawa vizimba Mkoa wa Mwanza kwa sababu hata hivi vizimba vimetengenezwa huko vikasafirishwa kuletwa Kigoma," alisisitiza.

Hata hivyo, Kali aliwataka wananchi kuwa wasimamizi na walinzi wa vizimba hivyo kwa kuwa wao ndio wanufaika wa mradi huo na amewataka viongozi wa wavuvi kushirikiana na viongozi wa seikali kufanya kazi hiyo kuwa rahisi na kuleta tija kwa jamii inayolizunguka Ziwa Tanganyika.

Baadhi ya wavuvi wilayani humo walitaja hatua hiyo kuwa muhimu kutokana na ziwa hilo kupungukiwa mazao ya samaki wakati mwingine wakipatikana samaki wachanga na baada ya kipindi hicho wanatarajia kupata wakubwa na wenye thamani kubwa.



## CBT yatoa onyo kwa wakulima wanaotorosha korosho

**Na Oscar Assenga,** TANGA

BODI ya Korosho Tanzania (CBT), mkoani Tanga imewaonya wakulima wenye tabia za kutorosha korosho kwenda kuuza nje ya nchi.

Imewataka wakulima hao kuacha mara moja kufanya hivyo ikisema siku zao zinahesabika kutokana na vyombo vya dola vinawatambua na watapokamatwa watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Moja ya athari za utoroshaji wa korosho kwenda nje ya nchi ni pamoja na kutokufikia malengo ya uzalishaji ikiwemo nchi mapato ambayo yangeweza kusaidia katika kuchochea maendeleo kwa wananchi wake.

Kaimu Meneja wa Bodi ya Korosho, Mkoa wa Tanga, Atufigwege Mwakyagi, alionya hayo wakati akizungumzia namna bodi hiyo ilivyojipanga kukabiliana na vitendo hivyo huku wakiwataka wenye tabia hizo kuacha mara moja

Alisema kwa kufanya hivyo maana yake ni kulihujumu zao hilo pamoja na juhudi za Serikali za kuhakikisha wakulima wanapata bei nzuri na bora ili kuweza kujikwamua kiuchumi kupitia kilimo hicho chenye tija.

"Ndugu zangu mnaotorosha korosho kufanya hivyo ni kosa na vyombo vya dola, hivyo tambueni siku zenu zinahesabika sisi kama bodi hatutakubali kuona watu wanahujumu zao hilo kwani zinatakiwa kumnufaisha mkulima na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ameweka nguvu kuhakikisha mkulima anapata bei nzuri na bora" alisema

Aidha alisema kwamba wale ambao wanafanya hivyo wanataka kufifisha juhudi za Serikali ambazo ni kuona wakulima wa zao hilo wananufaika nalo na hatimaye kuweza kujikwamua kiuchumi na kubadilisha maisha yao, hivyo hawatakuwa tayari kuona zinakwamishwa kwa namna yoyote ile.

Pamoja na mambo mengine alisema mauzo ya korosho msimu uliopita yalikuwa ni tani 741 kwenye mnada uliofanyika wilayani Mkinga na kufanikisha kuingiza Sh.milioni 703 ambazo wakulima wa zao hilo wameweza kunufaika nalo.

Akizungumzia suala la udhibiti ubora wa zao hilo alisema kwamba kwa sasa wamekuwa wakitoa mafunzo kwa wakulima ili kuweza kulima kilimo chenye tija.

Alisema pia wanadhibiti ubora ili kuhakikisha unakuwa mzuri kabla ya kwenda sokoni ambapo wamekuwa wakiuza kwenye mfumo rasmi.

# Makada CCM watishia kurudisha kadi kisa mgogoro wa mpaka

**Na Dege Masoli,** KILINDI

MGOGORO wa mpaka kati ya wilaya za Kilindi na Kiteto, umewagawa makada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), huku baadhi yao wakidaiwa kutishia kurejesha kadi za chama wakipinga alama mpya za mpaka.

Zaidi ya wanachama 6,000 walioko katika eneo la pembezoni unakopita mpaka huo wanapinga uamuzi huo wa serikali.

Akizungumza na waandishi wa habari mmoja wa wananchi hao, Ramadhan Juma, mkazi wa Kijiji cha Nkama, Kata ya Bokwa, Wilaya ya Kilindi mkoani Tanga, alisema wanachama 6,319 tayari wamejiorodhesha kurejesha kadi hizo kama serikali haitafanya marekebisho.

Alisema kata nyingine inayopinga mpaka huo mpya ni Mvungwe.

Kwa mujibu wa kada huyo, aliyejitambulisha kama mratibu wa zoezi hilo, alisema wanapinga kuanzishwa vijiji vipya vya wafugaji wa jamii ya kimasai vya Lolela na Losoiti vilivyopo wilayani Kiteto.

"Wanachama wanataka kurejesha kadi zao kwa kuwa wanaona kama serikali umekosea kushughulikia mgogoro huo kwa kufuata matakwa ya wakazi wa Wilaya ya Kiteto, ambao wengi wao ni jamii ya wafugaji kwa kuzalisha mpaka huo mpya unaowapa maeneo waliyokuwa wakiyatumia yawe malisho.

Diwani wa Kata ya Bokwa, Idrisa Mgaza, alisema kilichokosekana hapo ni wananchi kukosa elimu waliyopaswa kupewa kabla ya alama hizo kuwekwa.

Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Kilindi, Mohamed Kumbi, aliwashauri wanachama hao kutorejesha kadi zao, kwa kuwa kufanya hivyo kutawadhoofisha katika kufuatilia madai yao ngazi za juu.

Mkuu wa Wilaya ya Kilindi, Hashim Mgandilwa, alipoulizwa kuhusiana na malalamiko hayo alisema serikali imeshautatua na ulitangazwa kwenye Gazeti la Serikali la Novemba 17 mwaka jana baada ya kusainiwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

"Ndiyo kuna mpaka mpya umewekwa. Kwani tatizo ni nini mwandishi? alihoji Mgandilwa alipokuwa akizungumza kupitia simu yake ya mkononi....Unajua GN 853 ndiyo imefuta mipaka yote iliyokuwepo awali."

Mkuu huyo wa Wilaya, alisisitiza hao wanaolalamika ni watu wasiopenda kufuata mabadiliko hayo.



Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa, na Michezo, Hamis Mwinjuma (kushoto) akimkabidhi viti mwendo Mkurugenzi wa Shirika la Tanzania Health Awareness Foundation (TAHAF) wilayani Muheza, Musa Kinyasi kulia kupitia kampeni ya "Mtoto ni Tunu", Shirika hilo limekabidhi viti hivyo kwa watoto wenye ulemavu 10 wanaosaidiwa na shirika hilo ambavyo vilitolewa msaada na taasisi ya Silver Crescent kutoka nchini Uturuki. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Vijiji 10 vyapata dawa kudhibiti mabadiliko tabianchi

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

VIJIJI 10 vinavyokaliwa na jamii za kifugaji katika wilaya za Longido na Ngorongoro mkoani Arusha, ambavyo baadhi ya maeneo yake yanatishiwa na athari za mabadiliko ya tabianchi, wamepata 'mwarobaini' unaohimili tatizo hilo.

Ili kukabilina na hali hiyo, wameanza kuutumia mradi jumuishi wa mazingira na kuboresha maisha ya jamii, utakaosadia kurejesha uoto wa asili na vyanzo vya maji unaofadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Uhifadhi na Mazingira (IUCN).

Ofisa Program wa IUCN, Ng'walu Kidayi, jana alisema kuwa mradi huo pia utapita kwenye maeneo ya Ziwa Natron, Ziwa Eyasi na Bonde la Yaeda, linalokaliwa na makabila ya Wadatoga na jamii ya wawindaji, waokota matunda na warina asali ya Hadzabe.

Akizungumzia mradi huo ambao utashirikisha wananchi katika shuhguli zote zinazohusu uhifadhi endelevu, Mkuu wa Wilaya ya Longido, Marko Ng'umbi alisema: "Kwa bahati nzuri wilaya hii ina vijiji 49 na vyote vina ramani na vimepimwa."

Mratibu wa UCRT wa Wilaya ya Longido, Jamboi Baramayesu, alisema mradi huo unagharimu Dola za Marekani milioni 1.4 (zaidi ya Sh. bilioni tatu).


Kwa mujibu wa Baramayesu, mradi huo unatarajia kuvinufaisha vijiji 10 vya Wilaya za Longido na Ngorongoro.

Zaidia alifafanua: "Mradi huu unahudumia klasta tatu, ambazo ni klasta ya Ziwa Natron na Longido Magharibi, na klasta ya pili ni ya Ziwa Eyasi na Bonde la Yaeda, wakati ya tatu ni Simanjiro na Kiteto.

Kwa klasta ya Ziwa Natron na Longido Magharibi, vijiji vinavyopitiwa na mradi ni 10, kwa maana ya Ngorongoro vinne na Longido, vijiji sita."

Richard Mollel, alisema mradi huo ni rafiki kwao, na ni moja ya aina ya mradi unaotakiwa katika jamii ya kifugaji kutokana na kuwa shirikishi na unaojumuisha binadamu na wanyama.

Mkazi mwingine, Hellena John, alisema mradi huo unawapa fursa ya kushiriki katika kuhifadhi vyanzo vya maji, ambavyo vimekuwa vikivamiwa kwa namna moja ama nyingine kutokana na kutokuwepo kwa mipaka thabiti.



# Wakazi Ushetu waitwa kuchukua vitambulisho vyao vya taifa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa Kata ya Nyamilango Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wametakiwa kufuatilia vitambulisho vyao vya taifa katika ofisi za serikali za vijiji na kata.

Diwani wa Kata hiyo, Robert Mihayo aliyabainisha haya juzi wakati akipokea vitambulisho hivyo kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) Ofisi ya Kahama na kusema vitambulisho hivyo vitakuwa msaada katika mambo muhimu ikiwemo kutoa dhamana mahakamani.

Alisema amepokea vitambulisho 2,452 ambavyo watapewa wananchi kupitia Ofisi ya Mtendaji wa Kata, vijiji na vitongoji na kuwataka kujitokeza kuvichukua kwasababu umuhimu wake umeshaonekana tangu awali.

Alisema kwa wananchi ambao walikuwa na changamoto ya kukosa mikopo sasa wanauhakika wa kupata.

Mkazi wa Mhungula, Hamza Shabani alisema umuhimu wa kitambulisho hicho umekuwa mkubwa hususani katika shughuli za upatikanaji mikopo ambako wanahitaji kitambulisho halisi wala siyo namba.

Mkazi wa Mondo, Mayunga Mabala alisema yeye pamoja na mkewe hawakuwahi kupata namba wala kitambulisho, hivyo kwa sasa wanaendelea na hatua za awali kupata huduma hiyo.

Ofisa Usajili wa NIDA Kahama, Seriel Mchomvu alisema, wamepokea jumla ya vitambulisho 306,208 ambavyo vinakwenda kutolewa kwa wananchi wa Halmashauri ya Msalala, Ushetu na Manispaa ya Kahama na kuwataka wananchi kufika kwenye vituo walivyojiandikisha ili waweze kupata.

Alisema kwa wale ambao hawatavipata watambue kwamba uzalishaji bado unaendelea na utakapokamika watapewa kwa sababu vinatolewa kwa awamu.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha wote waliojiandikisha wanavipata ila kwa sasa wanaruhusiwa kuendelea kuzitumia namba walizopata katika mambo mengine hasa inapohitajika.



Mkuu wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Mboni Mhita akizungumza na wananchi wa kijiji cha Mitonga kata ya Nyamilangano halmashauri ya Ushetu, wakati wa mkutano wa hadhara wa kusikiliza na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi hususani katika sekta ya afya, maji, kilimo, elimu pamoja na miundombinu ya barabara juzi. **PICHA: SHABAN NJIA**

## Mbarawa atoa maagizo matatu kwa watumishi TAA

**Na Remmy Moka,** SAUT

WAZIRI wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa amewataka watumishi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Nchini (TAA) kuwajibika na kushirikiana katika utekelezaji kazi ili kuleta tija katika sekta ya uchukuzi.

Alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki wakati akifunga mkutano wa baraza la wafanyakazi la 31 katika sekta ya uchukuzi uliofanyika jijini Mwanza.

Mkutano huo ulikuwa na lengo la kubuni vyanzo vipya vya uongezaji wa mapato ya serikali na kuwavutia wawekezaji katika shughuli za kibiashara kupitia viwanja vya ndege hapa nchini.

Kadhalika aliwataka kuhakikisha wanasimamia utoaji wa huduma bora na zenye ufanisi kwa ndege na abiria wa ndani na nje ya nchi, ili kuwezesha utendaji kazi wenye tija katika sekta hiyo.

"Sambamba na hayo hakikisheni mnalinda miuondombinu ya viwanja vya ndege na kuifanyia matengenezo ya kinga mara kwa mara ili idumu kwa muda mrefu na kutimiza lengo la serikali la kuvifanya viwanja vyote kuwa vya kimataifa na kukidhi soko la ushindani duniani," alisema.

Kadhalika aliagiza mamlaka hiyo kuhakikisha wanabuni mbinu za kujiendesha kibiashara na kuvisaidia viwanja vya ndege nchini kuwa katika ushindani wa viwanja bora Afrika ikiwa ni sehemu ya kuwavutia wawekezaji wengi zaidi na kukuza sekta ya utalii na pato la taifa

Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), Mussa Mbura alisema mkutano huo ulijikita kujadili Mpango wa Bajeti wa 2024/2025, lengo likiwa ni kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo kumalizia ujenzi wa jengo la abiria katika Uwanja wa Ndege jijini Mwanza ambapo unatarajiwa kuhudumia abiria 1,000 kwa wakati mmoja.

# Mradi kuwawezesha wanawake kuongeza kipato wazinduliwa

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

MRADI wa kuwawezesha wanawake katika mnyororo wa thamani wa mazao ya uvuvi kwa nchi za Afrika Mashariki kupitia Ziwa Victoria umezinduliwa, utamwezesha mwanamke kuongeza kipato kupitia mazao hayo.

Akizungumza wakati wa kufunga mafunzo ya siku tatu ya Mtandao wa Wanawake Afrika Wanaojishughulisha na Uchakataji na Biashara ya Samaki (AWFISHNET), Mkurugenzi wa mradi huo, Suzanne Njeri alisema mradi huo utatekelezwa katika nchi za Tanzania, Kenya na Uganda.

Njeri alisema kuwa mradi huo wa majaribio utatekelezwa kwa kipindi cha miaka miwili na nusu na mpango ni kuwafikia wanawake 5,000 Afrika Mashariki, ambapo kwa kila nchi watakuwa wanawake 1,667.

Alisema mradi huo utakuwa na mambo mbalimbali ya kumuwezesha mwanamke lakini kubwa zaidi ni kumuinua kuanzia pale alipo ili aweze kuongeza uzalishaji wa mazao ya uvuvi.

Ofisa Uvuvi Mkuu kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Jovice Mkuchu alisema wizara imeweza kufanya tathmini mbalimbali kwenye sekta ya uvuvi, ambapo mradi unaenda kutatua changamoto za wanawake katika kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi tangu yanapovuliwa.

Aidha, alisema wizara inashukuru uwepo wa mradi huo ambao umeona umuhimu wa kuwainua wanawake wa Tanzania katika Sekta ya uvuvi kwa kuwa wizara ni mlezi wa mtandao wa Wanawake Wanaojishughulisha na Uvuvi Tanzania (TAWFA) na kwamba wizara itakuwa bega kwa bega kuwezesha mradi huo kuwa na tija.

Mshauri Mkuu Elekezi wa mradi huo, Editrudith Lukanga alisema mradi unafadhiliwa na taasisi ya Bill and Melinda Gates kwa Dola za Marekani milioni 1.5 na utakuwa wezeshi kwa kuwa umewashirikisha wadau kuanzia ngazi ya chini.

Alisema katika utafiti walizofanya kwenye mialo mbalimbali wamebaini wanawake wamechukulia zao la samaki kama biashara, huku wakiwa na upungufu mkubwa wa wao wenyewe katika ulaji wa samaki na kukimbilia kuuza na kupata fedha ili wanunue chakula kingine au kununua mahitaji mengine ya familia. Alisema kumekuwa pia na changamoto ya upatikanaji wa rasilimali fedha kama mtaji ili kuwasaidia wanawake kununua bidhaa kwa kiwango kikubwa ili kukidhi ushindani sokoni.

Pia, alitaja upotevu wa samaki kabla ya kuwafikisha sokoni baada ya kuvuliwa imekuwa ni changamoto kwa wanawake.

Mradi wa kuwawezesha wanawake katika mnyororo wa thamani wa mazao ya uvuvi Afrika Mashariki kwa sasa unatekelezwa kupitia Ziwa Victoria, lengo likiwa ni kufikia maeneo mengine ya Afrika ambayo yana maji ya asili ikiwemo bahari na maziwa.



Ukurasa 12

BITEKO AKICHANGIA YAKE:

**GPETSP, Mradi unaofukua na kumaliza kero zao walimu ziliko**



Ukurasa 13

Mjue Deo Manjiwa, mfugaji njiwa mapambo, akiuza hadi Sh. 400,000

Nipashe

# TESA

Jumanne Aprili 2, 2024

TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 14

BENKI ILIPOTUA SHULENI BUSIYA...

**Ufadhili vyoo, chumba kusitiri hedhi vyamaliza vilio vya mabinti miaka 17**

ELIMU
NA PETER ORWA

AWAMU SITA & UKOMBOZI DARASANI...

# Siri ya kinachoendelea mtaala mpya, Elimu Kujitegemea na safari mafanikio

HADI sasa inashuhudiwa mageuzi makubwa katika Awamu ya Sita, chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kuboreshwa tija katika muundo na maudhui ya elimu shuleni nchini. Sasa, elimu ya chekechea ni lazima, vivyo hivyo mpaka kidato cha nne.

Pia, anayejiunga elimu ya msingi; darasa la kwanza ukomo uko darasa la sita, darasa la saba limeondolewa, sambamba na maudhui ya masomo kuboreshwa, ikiwamo lugha inayotumika, pia masomo mapya.

Kwa ujumla, kila mahali hitaji elimu duniani lina nafasi yake. Mwenendo wa maisha ya kila siku kwa ngazi zote na mahali pote, elimu inahitajika.

Vilevile, ili jamii hiyo iboreshe maisha yake inahitaji maendeleo ambayo kimsingi mwanazuoni mzaliwa na raia wa Guyana, Profesa Walter Rodney, aliyefundisha katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, akaandaa tafsiri kitaaluma kuwa ni mabadiliko ya viwango; ubora na idadi kuelekea kuzuri zaidi.

Vivyo hivyo, wasomi hao wanabainisha elimu inajumuisha sehemu ya maendeleo kwa ujuzi, maarifa na ufahamu anaoupata mtu kumudu mazingira aliyo nayo. Elimu daima ina mustakabali mpana kila mahali ipo, maana maisha ya mtu yanaendana na ufahamu pia matumizi yake, huku huo ujuzi na maarifa wa mtu anautumia kama nyenzo ya kuwajibika.

Kwa ujumla, nafasi ya elimu ina sura mbili, rasmi na isiyo rasmi. Elimu isiyo rasmi mtu hupewa ujuzi na maarifa, mahsusi kukidhi mazingira na utamaduni wake.



Darasa la Elimu ya Watu Wazima likiendelea. **PICHA: MTANDAO**

Rasmi husimamiwa na mtaala, ambao ni mpango mkuu wa elimu kukidhi malengo yake ndani yake ndio kuna muhtasari wa masomo (syllabus), unaowaongoza kwa kile kinachopaswa kufunzwa katika kipindi husika.

**NGUZO ZAKE ZILIVYO**

Mfumo wa elimu unaundwa na nguzo kuu nne; shule, msimamizi mkuu -serikali, wazazi au walezi na wadau, wote wanatarajiwa kushirikiana kufanikisha kile anachofunzwa mwanafunzi.

Shule huendana na mambo makuu matatu, ambayo ni miundombinu ya majengo, samani za shule, hata vitabu kwa kutumiwa na walimu, pia wanafunzi.

Nafasi ya mwanafunzi ni kusikiliza darasani na kujifunza maelekezo ya mwalimu akitumia mbinu mbalimbali anazoelekezwa na mwalimu, akiwa katika hadhi ya uanafunzi na mtoto katika familia ya shule.

Mwanafunzi huyo ambaye sehemu kubwa ya maisha yake yako shuleni, anakuwa 'mtoto wa shule'. Moja ya nguzo kuu inayomuongoza ni nidhamu ya jumla, pia kutii sheria za jumla za mwanafunzi kitaifa, pia mahsusi kwa shule tajwa.

Hapo msimamizi mkuu mwalimu anayesimamia kufundisha, anaelekeza na kuwalea wanafunzi. Hiyo ndio maana, maudhui ya mafunzo ya walimu, mbali na stadi za somo analofundisha, pia hujifunza; falsafa, sosiolojia, saikolojia za mwanafunzi, pia usimamizi wake na masomo.

**MZAZI NYUMBANI**

Mdau mzazi wa mtoto aliyeko shuleni, ndiye mshirika wa kwanza wa shule na katika lugha rahisi 'mzazi ni mwalimu wa mtoto nyumbani.'

Katika dhamira ileile aliyotambua hata akampeleka mtoto masomoni jambo la kwanza anawajibika nalo ni kukidhi mahitaji yote kutoka shule na yale yanayomuwezesha mtoto kusoma.

Mbali na Sheria ya Elimu, pia Sheria ya Mtoto ya 2009, inamuwajibisha mzazi kuhakikisha mtoto anapata elimu msingi iliyo mbele yake, ikiwamo kugharamia na kusimamia mtoto.

Hiyo kisheria inaendana na mahitaji ya kiafya na malezi ya jumla yanayoendana na kufanikisha elimu, hasa katika wajibu wa kumlea mwanafunzi shuleni na nje ya masomo.

Mfano uko katika shule na mzazi kushirikiana kutumia mwongozo wa kiserikali kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), mwanafunzi anapatiwa huduma hiyo, afanikishe kusoma kwa amani.

**DIRA SERIKALINI**

Ikirejewa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 ni ya kuwa na taifa la watu wenye elimu ya kati na ya juu ili kuwa na watendaji kazi wenye uwezo wa kushughulikia kikamilifu changamoto za kimaendeleo.

Hapo inatoa tafsiri ya msingi ya wajibu wa serikali unaopatikana katika Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014, yaliyofanyiwa mapitio mwaka jana, inataja dira, dhima na malengo ya sera.

Kwa mujibu wa sera hiyo, msingi wa elimu na mafunzo utajikita katika kumjengea Mtanzania misingi bora ya malezi, maadili, ujuzi, umahiri na kumuwezesha kujitegemea.

Hapo inamaanisha nadharia ya 'Elimu ya Kujitegemea' ambayo ni andiko la mwaka 1967 la mwasisi wa taifa, Mwalimu Julius Nyerere, akaitafsiri aina ya elimu anayopaswa kuipata Mtanzania inaendelea kudumishwa hadi katika elimu ya sasa.

**INAENDELEA UK.13**

ELIMU NA SABATO KASIKA

BITEKO AKICHANGIA YAKE:

# GPETSP, ni mradi unaofukua na kumaliza kero zao walimu ziliko

• Waziri Mkenda: Inawagusa kila kona

HIVI karibuni, ilizinduliwa Programu ya Kuboresha Kada ya Ualimu nchini (GPETSP), ambavyo mgeni rasmi alikuwa Naibu Waziri Mkuu, Dk. Dotto Biteko.

Akihutubia wakati wa uzinduzi wa programu hiyo jijini Dar es Salaam, kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan, anasema uwekezaji wowote katika sekta ya elimu, lazima umguse mwalimu.

Kwanini? Anataja sababu kuwa mwalimu diye injini, ndiye kiongozi wa rasilimali zote zinazowekwa kwenye mfumo wa elimu nchini.

Anasema mwalimu ni rasilimali inayofanya rasilimali nyingine ziweze kuleta matokeo chanya kwenye sekta ya elimu.

Naibu Waziri Mkuu kwa niaba ya Rais, anasema serikali inatambua umuhimu wa walimu na kwamba kutokana na kutambua umuhimu wa walimu, serikali imekuja na programu hiyo kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

Aidha, anasema katika jitihada za kuendelea kutambua mchango wa mwalimu, kwa sasa kuna ongezeko la ajira kwa walimu, madaraja na pia bajeti ya elimu imeongezeka. Lingine anaeleza anachotamani ni kwamba, walimu wawe na siku maalum ya motisha, kwa kutambua mchango wao katika sekta ya elimu.

"Mwalimu ni rasilimali kuu inayofanya rasilimali nyingine ziweze kuleta matokeo chanya. Kwenye sekta ya elimu, ndio maana mtaona programu tunayoizindua leo inaonyesha kwa vitendo kuwa serikali tunatambua kwamba lazima tuwekeze zaidi kwa walimu.

"Kwenye mazingira ya kujifunza na ufundishaji, pia kuwatambua walimu kuwa ninyi ndio watu tunaowategemea kufanya elimu yetu iweze kwenda mbele," anatamka Dk. Biteko, ambaye naye si haba, amekaa darasani vilivyo.

Anasema, hadi sasa rais anafanya kila jitihada katika yanayowahusu walimu, yafanyiwe kazi kwa kasi, ikiwamo kuwapunguzia kero zinawazowakabili, ili wajikite kufundisha na kutatua changamoto za wanafunzi shuleni.

### UFAULU KUONGEZEKA

Anasema, kutokana na kazi nzuri ya walimu ufaulu wanafunzi, kutoka shule ya msingi kwenda sekondari umeongezeka kutoka 907,802 mwaka 2021 hadi 1,092,984 mwaka 2023 ikiwa ni ongezeko la asilimia 20.4.

"Serikali inaendelea kuboresha bajeti ya elimu na kwamba katika mwaka 2021 fedha iliyotolewa ilikuwa ni Sh. Trilioni 4.7 na kwa mwaka 2023 imeongezeka hadi Sh. Trilioni 5.7 sawa na asilimia 20.4," anasema.

Kwa upande wa ajira za walimu, zinatajwa kuongezeka katika kipindi cha serikali ya awamu ya sita, walimu 37,473 wa sekondari na msingi wameajiriwa, walimu 227,383 wamepandishwa madaraja na walimu 20 wamebadilishiwa vyeo.

Hata hivyo, anasema bado kuna changamoto kwenye sekta ya elimu, ikiwamo ya kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi ambao unahitaji ongezeko la walimu na miundombinu mingine, ikiwamo madarasa na nyumba za walimu.

"Serikali inatambua bado kuna kazi kubwa ya kufanya katika sekta ya elimu na ninatoa wito kwa wadau kushirikiana na serikali, ili kuimarisha mahitaji ya elimu nchini," anasema.

Anafafanua kuwa serikali ya awamu ya sita inawajali walimu na kwamba ndio maana, inatekeleza vipaumbele nane ili kuboresha kada hiyo.

Anavitaja baadhi ni ujenzi wa nyumba za walimu kwenye halmashauri za pembezoni; kuimarisha mfumo wa motisha kwa walimu ili kuwafanya wabaki kwenye kazi yao.

> "Serikali inatambua bado kuna kazi kubwa ya kufanya katika sekta ya elimu na ninatoa wito kwa wadau kushirikiana na serikali, ili kuimarisha mahitaji ya elimu nchini.



Naibu Waziri Mkuu, Dotto Biteko

"Vilevile, inawezekana kuandaa mfumo jumuishi wa kielektroniki wa uandaaji, usimamizi na upangaji wa walimu kwa kuzingatia usawa wa kijinsia na kuwezesha utekelezaji wa mpango wa ajira kwa walimu wa kujitolea ili kupunguza kero za upatikanaji wa walimu wa msingi ili kuimarisha mazingira ya kujifunza na ufundishaji.

"Vipaumbele vingine ni kumuwezesha mwalimu kufanya upimaji wa kielektroniki, ili kupata matokeo ya kila hatua ya kujifunza, kujenga vituo vya walimu na kuweka samani na vifaa vya kielektroniki," anasema.

Dk. Biteko akimwakilisha Rais, anasema serikali inachukua hatua ikiwamo kuwezesha mafunzo endelevu kwa walimu walio kazini, ununuzi wa zana na vifaa visaidizi kwa wakufunzi, walimu, walimu tarajali na wanaofundisha wanafunzi

Pia, kuna wenye mahitaji maalumu wanayotoa ufadhili wa masomo kwa walimu wanaofundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum.



Walimu wa shule wakiwa katika mafunzo ya maendeleo kazini. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

### SALAMU ZA PONGEZI

Naibu Waziri Mkuu Biteko, anampongezea Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Kimataifa inayoshughulikia Masuala ya Elimu Duniani (GPE), kwamba nafasi aliyo nayo ni heshima kwa nchi.

"Nafasi hiyo pia ina heshima kwa sekta ya elimu nchini, kwani amekuwa na mchango katika kuhakikisha nchi inafaidika na mfumo wa GPE, ambao unahudumia nchi 89 duniani," anasema.

Aidha, anaiagiza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na ile ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, kuangalia utaratibu bora wa kuwapa motisha walimu kwa kutenga siku moja ya kuwapa motisha badala kusubiri Mei Mosi, lengo ni kupata matokeo bora kwenye sekta hiyo ya elimu.

Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Rais Mstaafu Kikwete, anasema lengo la taasisi hiyo ni kusaidia kuchochea maendeleo ya elimu katika nchi 89 zinazoendelea, hasa za kipato cha chini na za kipato cha kati ikiwamo Tanzania inayonufaika na GPE.

"Tangu GPE ianzishwe mwaka 2002, imeshachangia Dola za Marekani milioni 330 nchini Tanzania na inaunga mkono juhudi za serikali kuboresha sekta ya elimu ili kila mtoto nchini awe na ujuzi na maarifa na sasa taasisi hii imeidhinisha ufadhili wa Dola za Marekani milioni 80 kwa ajili ya programu ya GPETSP," anasema Kikwete.

### WAZIRI MKENDA

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda anasema, programu ya GPETSP, inagusa sehemu mbalimbali katika kada ya ualimu, ikiwamo kuhakikisha kuwapo utoshelevu wa walimu, ubora, miundombinu, vitendea kazi na kuendeleza makazi ya walimu na motisha kwa walimu.

"Serikali imekuwa ikiyafanyia kazi masuala hayo, lakini GPETSP inakuja kuongeza nguvu na kasi ya utekelezaji wa programu za serikali ikiwamo Sera ya Elimu," Prof. Mkenda anasema.

ELIMU
NA MWANDISHI WETU

# Mjue Deo Manjiwa, anafuga njiwa mapambo, akiuza hadi Sh. 400,000

## • Anena: Najisikia 'ubahili' kuwachinja

KWA wengi njiwa ni kitoweo na hufugwa kwa mapenzi, si biashara. Lakini Deogratius Temba, kijana kutoka Dodoma, Tanzania amebadilisha dhana hiyo. Anafuga njiwa wa kipekee.

Hao ni njiwa wanaojulikana kama wa mapambo, wanaotumika kupendezesha makazi, ofisi au sehemu zingine kama hoteli na pa kupumzikia. Deogratius ana zaidi ya aina 10 ya njiwa wa mapambo, kila mmoja anauzwa kati ya Dola za Marekani 85, mpaka180, au Sh. laki 4 za Tanzania.

Mtu anaweza kujiuliza, wanafananaje njiwa hao, na kwanini kijana huyo maarufu kama Deo Manjiwa, ameamua kuwafuga njiwa hawa wa mapambo?

### HISTORIA YA NJIWA

Ufugaji wa njiwa ulianza miaka zaidi ya 5,000 iliyopita. Njiwa walifugwa kienyeji na kawaida. Waliwafuga kwa madhumuni tofauti, ikiwamo kutumika kama kitoweo, baadhi kuwatumia kupeleka ujumbe vikaratasi ama kufika kwao, wakifundishwa kwa namna mbali mbali.

Lakini katika kipindi cha miaka 50 iliyopita, ufugaji njiwa kwa mapenzi au kwa kujifurahisha ulianza kushika kasi na sasa karibu kila mahali, ufugaji huo na ule wa kibiashara umeanza kushika kasi.

Deo Manjiwa anaeleza:"Wakati nataka kuanza kuwafuga hawa njiwa majirani hawakuwa na shida ila mke. Shida ilikuwa kwa mke wangu.Kwa sababu wakati nataka niwanunue, mke wangu aligoma kabisa."



Deo Manjiwa, akihudumia njiwa wake. **PICHA: MTANDAO**

### ULAJI WAO BALAA

Tofauti kubwa ya njiwa hawa wa mapambo iko kwenye maeneo manne. Ulaji wao, maisha yao, mwonekano wao na kustahimili, kwao ugumu wa mazingira.

Wana mwonekano mzuri unaobebwa na rangi zao, muundo wa maumbo yao, manyoya na namna wanavyotembea. Hicho kinawatofautisha na njiwa wengine wa kawaida wa asili.

Hao walivyo, hawawezi kuvumilia mazingira magumu. Lakini wanapowekwa kwenye mazingira bora huzaliana sana. Deo Manjiwa anasimulia, ndani ya mwaka mmoja amefanikiwa kuzalisha mamia ya njiwa kutoka njiwa sita tu alioanza nao.

Mbali na magonjwa ya mafua kama wanavyoumwa njiwa wengine, Deo analalamika tu ulaji mkubwa wa njiwa hao.

"Na hao wa siku wanaweza kula kilo tano au nne (za nafaka)," anasema, huku akiongeza kuna aina ya ulaji unaomtisha. Mmoja wa watu waliofika kushangaa njiwa hawa nyumbani kwa Deo Manjiwa, oneo la Makole, Dodoma, akatamka: 'Wanakula kama mchwa, kilo tano si mmekula familia wiki nzima."

### BIASHARA NJIWA

Manjiwa anathibitisha njiwa ni biashara kubwa, yeye akianza na mtaji wa njiwa sita tu kutoka Zanzibar. Sasa ana mamia ya njiwa wenye thamani ya zaidi ya milioni 25 za akitaja sawa na wastani wa Dola za Marekani 10,000.

"Njiwa wote hapa tukiwauza kwa shilingi za Kitanzania 200,000 labda tuseme wako njiwa 100. Laki mbili mara mia inakuja milioni 20. Lakini kila 200,000 ukiziweka kwa gharama za mchele wa sasa hivi unapata kilo 66.

"Kilo 66 kwa familia ya watu wanne au watano wanaweza wakala kilo moja. Kwa hivyo, thamani ya njiwa mmoja ya Shilingi 200,000 inaweza kulisha familia kwa miezi miwili. Kwa hiyo njiwa sio mapambo tu njiwa pia ni kipato," anaeleza.

Pai, anafafanua bei ya mchele kijijini isiyozidi Shilingi 2,500 kwa kilo, njiwa anayeuzwa Shilingi 400,000 anaweza kutoa zaidi ya kilo 100 za mchele.

### HUWA WANALIWA?

Deo Manjiwa anawaeleza, ni njiwa wanaoliwa kama wengine. Tena kwa sababu ni wakubwa kwa maumbo, wapo wanaofikia maumbo ukubwa kama wa kuku wa kawaida.

"Huwa nawachinja sana, hasa wale wenye rangi ambazo naona sokoni hazitavutia au wanaoumwa', anasema, ingawa ana ufafanuzi hapendi kufanya hivyo kwa sababu ya thamani yao.

"'Yaani njiwa wa (shilingi) 400,000 umchinje tu?" anahoji Deo, huku akiendelea kuwahudumia njiwa wake kwenye mabanda yake mawili makubwa.

• ***Kwa mujibu wa BBC.***

# Siri ya kinachoendelea mtaala mpya, Elimu Kujitegemea, safari yake

INATOKA UK.11

Sera mpya iliyobuniwa katika zama za Awamu ya Sita na kuanza kutumika mwaka huu, inaelekeza Elimu ya Kujitegemea, itaendelea kuongoza utoaji elimu na mafunzo kwa kuzingatia mabadiliko yanayotokea katika jamii, kisiasa, kiuchumi, kisayansi na kiteknolojia.

### ELIMU YA KUJITEGEMEA

Nadharia hiyo ya Elimu ya Kujitegemea ipatikanayo katika maandiko kama ya kitabu cha Ujamaa Essay, inaelekeza sura inayopaswa kuwamo katika elimu ya Kitanzania.

Moja, ni kwamba maudhui ya mitaala na elimu itolewayo, irejee katika uhalisia wa maisha ya Kitanzania. Hapo ikawa sababu mojawapo katika elimu ya msingi ikaendeshwa kwa lugha ya Kiswahili.

Pia, ndio mtazamo wa taaluma mpya, mkazo unawekwa katika masomo ya teknolojia, huku Historia na Maadili ikifunzwa kwa Kiswahili katika ngazi ya msingi, ikiwa ni mahitaji ya sasa.

Eneo lingine la Elimu ya Kujitegemea, inabeba tafsiri Mtanzania anapoelimika anakuwa mnufaika wa elimu ya Kitanzania, hata anaanguka na dhana alichokivuna ujuzi na maarifa anarejesha kwa jamii yake, ikiwamo kutoa msaada wa ujuzi na maarifa inapobidi.

Mfano hai ni katika miaka ya 1970, ilipobuniwa Kisomo Chenye Manufaa (kujifunza kusoma na kuandika) baada ya Azimio la Musoma, 1974, kasoro ya walimu ilizibwa kwa kiasi kikubwa na waliosoma wakajitolea kuwa walimu vijijini kwa mafanikio. Ni aina ya msaada ulioshuhudiwa kwa kiasi kikubwa vijijini.

Vilevile, lengo la maudhui ya elimu nchini linataka iunde stadi na uelewa wa anayesoma kumudu na kukidhi matatizo na mahitaji yake.

Huko nyuma katika Muhtasari wa Masomo wa 1976, ukawa na masomo ya Maarifa ya Nyumbani na Elimu ya Siasa, ambayo baada ya mageuzi ya mwaka 1992, Elimu ya Siasa nafasi yake ikachukuliwa somo Uraia, huku katika kidato cha Sita 'General Studies.

Vilevile sekondari kukawapo mchepuo wa: Kilimo, Biashara, Sayansi na Ufundi, ambao unadamu, lakini kukiwepo masomo mapya ya kidini, pia Kichina.

Pia, Elimu ya Kujitegemea inahimiza kila ngazi ya elimu kama vile, shule ya msingi, sekondari kidato cha nne, pia cha sita na ngazi mbalimbali za elimu ya vyuo inapaswa kujitegemea na si kuhesabiwa mhusika 'amefeli.'

Sababu kubwa ni ngazi hiyo aliyoipata msomaji itumike kwa msomo kuhudumia mahitaji yake kimaisha. Hiyo inaendana na

INAENDELEA UK.14

ELIMU

NA MARCO MADUHU,
KISHAPU

## BENKI ILIPOTUA SHULENI BUSIYA...

# Ufadhili vyoo, chumba kusitiri hedhi vyamaliza vilio vya mabinti miaka 17

BADO katika jamii kuna shida namna ya kuhudumia mabinti wakiwa kwenye hedhi, ndani ya mazingira shuleni. Hivyo, kunasisitizwa umuhimu wa kuwapo chumba maalum cha huduma hiyo shuleni.

Pindi huduma hiyo inapokuwa duni, daima mwanafunzi huishia katika mgumu hata kukosa baadhi ya ratiba na kimasomo.

Kwa sasa, wanafunzi wa kike katika Shule ya Sekondari Busiya wilayani Kishapu, wanasimulia namna wanavyokosa vipindi vya masomo darasani wanapokuwa katika siku zao za hedhi, kutokana na shule hiyo hapo awali kutokuwa na chumba maalumu cha kujistiri hedhi.

Wa kwanza (jina tunalo), mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Busiya wilayani Kishapu, anasema shule hiyo ilianzishwa mwaka 2007 na haikuwahi kuwa na chumba maalumu kwao kujisitiri.

Muda mrefu ukapita, hadi kupatiana msaada kutoka kwa Benki ya Biashara Tanzania (TCB) Tawi la Shinyanga, ilipowajengea mabinti masomo kupata huduma hiyo, kwani mbadala wao huko nyuma kujisitiri, mwanafunzi huyo anasimulia ilikuwa kutimiza utoro wa masomo, hadi wanapokuwa sawa.

Anaeleza kwamba shule hiyo awali ilikuwa na shimo moja la choo lenye matundu sita, matatu wanatumia wavulana na matatu wasichana, tena wanajisaidia sehemu moja kwa kugawana matundu hayo na hakuna huduma ya maji na vyoo vikibaki vichafu.

"Wanafunzi wa huku vijijini ni tofauti na wa mjini. wenzetu wana uwezo wa kupata taulo za kike, lakini sisi wengi hutumia... kujistiri hedhi ambayo huwezi kukaa nayo hadi jioni, lazima ulibadilishe..." anasema.

Anaongeza: "Wanafunzi wa kike huwa watoro hatuji shule na kukosa vipindi darasani na kufanya vibaya kitaaluma hasa masomo ya sayansi."

Mwanafunzi mwingine, Fredina Masanja, anasema baada ya kujengewa chumba maalumu cha kujistiri hedhi, utoro wao utatoweka na hawatakosa vipindi darasani, wakitarajia kufanya vizuri Kitaaluma.




Vyoo vipya vilivyojengwa katika Shule ya Sekondari Busiya wilayani Kishapu. **PICHA: MARCO MADUHU**

### MKUU WA SHULE

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Busiya, Badi Mfinanga, anasema shule hiyo ina jumla ya wanafunzi 351, wavulana 176 na wasichana wako 175, huku matundu ya vyoo yaliyokuwapo awali ni sita, wala hapakuwapo chumba maalumu kujistiri hedhi, akilalamika mabintio shuleni walikuwa watoro, hata kusababisha wakashuka kitaaluma.

"Matokeo ya kidato cha nne ya mwaka jana yalikuwa siyo mazuri sana, na hii ilisababishwa na Utoro wa wanafunzi, ambayo daraja la kwanza alipata mwanafunzi mmoja, la pili wanafunzi watatu, daraja la tatu wanafunzi wanne, daraja la nne wanafunzi 34 na 'Ziro' (sifuri) wanafunzi 38.," anasema Mfinanga.

### MFADHILI ANENA

Meneja wa Benki ya TCB, tawi la Shinyanga, Julius Mataso, anasema mwaka 2021 alikaribishwa kuwa mgeni rasmi katika Shule ya Sekondari Busiya na akakumbana na hali mbaya ya vyoo na namna ya kujisitiri mabinti.

Anasema, aliguswa na hali hiyo na kuamua kutoa sehemu ya faida wanayoipata, kuwajengea matundu 12 ya vyoo kikiwamo na chumba maalumu cha kujistiri hedhi, ili wasichana wasikose vipindi vya masomo darasani au kutaabika.

"Ujenzi wa matundu haya 12 ya vyoo, ambayo sita watatumia wavulana na sita wasichana pamoja na chumba maalumu cha kujistiri hedhi ,tulianza ujenzi wake Oktoba mwaka jana na umekamilika Februari mwaka huu kwa gharama ya shilingi milioni 33.7," anafafanua Mataso.

### DEO & DIWANI

Ofisa Elimu Sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, David Mashauri, anasema ukosefu wa vyoo bora shuleni pamoja na chumba maalumu cha kujistiri hedhi, ni changamoto kubwa katika safari ya elimu kwa wanafunzi kutosoma katika mazingira rafiki.

Anasema serikali imekosa uwezo wa kutekeleza mahitaji yote ya wanafunzi shuleni, na kwamba hiyo ndiyo fursa ya wadau kuiunga mkono serikali changamoto zinazoikabili sekta ya elimu, ikiwamo upungufu wa matundu ya vyoo na chumba cha kujistiri hedhi.

"Mahitaji ya Matundu ya vyoo kwa shule za sekondari wilayani Kishapu ni 520. Yaliyopo 274 na upungufu ni 246. Tupo pia kwenye ukamilisho wa matundu ya vyoo 33 na tunazingatia ujenzi wa chumba maalumu cha kujistiri hedhi wanafunzi wa kike," anasema Mashauri.

Anafafanua kwamba, serikali imeshatoa kiasi cha fedha shilingi milioni 75, zinazotumika kujenga matundu ya vyoo 75 kupunguza pengo la upungufu uliopo.

Diwani wa Itilima wilayani Kishapu, Lameck Nsumbata, anasema suala hilo la ujenzi wa vyoo shuleni na chumba maalumu cha kujistiri hedhi, itakuwa ni ajenda ya kudumu kwenye vikao vya Kata, ili kuhamasisha wananchi kuanzisha ujenzi wa vyoo na kisha Serikali kuvimalizia.

Anasema ujenzi wa chumba maalumu cha kujistiri hedhi ni muhimu pia hata kwa shule za msingi, ambapo huko hakuna kabisa.

## Siri ya kinachoendelea mtaala mpya, Elimu Kujitegemea, safari yake

**INATOKA UK.13**

kigezo cha mwisho cha Elimu ya Kujitegemea kwamba maudhui hayo aliyobuni Mwalimu Nyerere, inachukua nafasi hadi leo isimuandae kwa ajili ya ajira ofisini pekee, bali stadi za kazi yoyote.

Ni kilio kilichotawala kwa wadau wengi katika hitaji hilo, huku Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, mbali na kuliweka katika mtaala wake mpya, pia ameuonyesha kwa vitendo kupitia Shamba Darasa la Vijana lililopo mkoani Dodoma.

### SERA MPYA

Yafuatayo ni baadhi ya malengo kuelekea elimu ya Kitanzania katika mwelekeo ujao, baada ya kubarikiwa na Rais Samia Suluhu Hassan:

• Serikali itahakikisha kuwapo miundombinu bora

na stahiki ya kutosheleza mahitaji ya elimu na mafunzo

kwa makundi yote katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

• Serikali itahakikisha kuwa huduma muhimu zikiwamo za chakula bora, mawasiliano, umeme, maji safi na salama, na afya zinapatikana katika shule na vyuo.

• Serikali itahakikisha kuwapo mazingira bora na yenye usalama katika utoaji elimu na mafunzo.

• Utawekwa utaratibu wa kuhakikisha muda wa

kukamilisha elimu na mafunzo katika ngazi mbalimbali za elimu baada ya elimu msingi, unalenga mwanafunzi kupata ujuzi stahiki kulingana na mfumo wa tuzo wa taifa.

### WADAU WA ELIMU

Kundi la mwisho katika kutanikisia elimu ni wadau na ndio maana hata katika sera mpya, bado inakazia ushirikishwaji wao kufanikisha elimu.

Hapo inajumuisha umma, unaowasimamia wanafunzi kuwa 'watoto wao' kila kona, wakichangia kuwafanikisha kitaalamu, hali kadhalika wadau kama wasomi na makada wake, mahsusi walimu na wanataaluma wenzao, kama wa maabara shuleni.

**• Jumanne ijayo, kilichomo katika stadi za mafanikio na kukwama darasani; Mwalimu Vs Mwanafunzi.**



# UNESCO yatoa mil.100/- ukarabati vituo vya afya katika vyuo vikuu

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) limetoa Sh. milioni 100 kwa ajili ya kukarabati vituo vya huduma za afya katika vyuo vikuu vitatu ikiwemo Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Akizungumza juzi wakati wa hafla ya makabidhiano ya ukarabati wa vituo vya afya vya UDOM, Mkuu wa UNESCO, Dar es Salaam, Michel Toto wanaunga mkono juhudi za serikali na wadau mbalimbali wa elimu na afya.

Alisema lengo ni kuwezesha vijana waliopo masomoni kupata elimu na huduma sahihi za afya na ustawi ili waweze kustawi na kufikia malengo yao ya elimu na kuweza kuleta mchango chanya kwenye jamii na taifa.

Alisema UNESCO kupitia mradi wake wa 'haki zetu, maisha yetu, mustakabali wetu' unaofahamika kama O3 plus umesaidia ukarabati wa vituo vya huduma za afya katika vyuo vikuu vitatu ikiwemo UDOM, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu (DUCE).

Alisema katika UDOM mradi wa O3 plus umewezesha uboreshaji wa mazingira ya vituo vya afya vinavyopatikana chuoni hapo ikiwemo kutengeneza vyumba vinne vipya vya madaktari.

Pia, alisema kukarabati wodi mbili za wagonjwa, ukarabati wa vyoo, ununuzi wa vifaa mbalimbali kama vile mabenchi ya kisasa ya kukalia wagonjwa wakiwa wanasubiri kumuona daktari, luninga ambazo huwekwa vipindi vya afya na kuwezesha wagonjwa kupata elimu na kuboresha sehemu ya mapokezi ya wagonjwa.

Naibu Makamu Mkuu wa Taaluma, Utafiti na Ushauri, Profesa Razack Lukina aliishukuru UNESCO kwa uboreshaji wa miundombinu ambayo itasaidia utolewaji huduma kwa wakati.

Mganga Mfawidhi Hospitali ya UDOM, Dk. Matobogolo Boaz alisema kuwa maboresho yaliyofanyika yatasaidia kuboresha utoaji wa huduma za afya.

Alisema hospitali hiyo iko katika ngazi ya wilaya, ina sehemu tatu za kutoa huduma na inahudumia watu 36,000.

Alisema kutokana na ongezeko la idadi ya watu kuna maboresho ambayo yanahitajika ili kuendana na ongezeko la idadi ya watu.

Mtaalam wa Afya na Elimu ambaye pia ni Mratibu wa Programu kutoka UNESCO, Mathias Luhunya alisema mradi wa O3 plus umekuwa ukitekelezwa kwa kipindi cha miaka miwili, hadi sasa upo katika vyuo vikuu 17 Tanzania Bara 15 na Zanzibar viwili.

Mmoja wa wanafunzi wa UDOM, Fransisco Mushumbuzi alisema amekuwa ni miongoni mwa vijana 100 waliopewa mafunzo ya uelimishaji rika na afya ya uzazi.

Alisema kuwa kuboreshwa katika kituo hicho cha afya kutaboresha utendaji na wananchi watapata huduma kwa wakati.



Ofisa Uendeshaji, Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar, Rajab Uweje, (aliyesimama), akizungumza wakati wa ziara ya kutembelea vituo vya watu wenye mahitaji maalum, na watoto yatima jijini Dodoma, kama sehemu ya matendo ya huruma yaliyoambatana na kugawa mahitaji mbalimbali ikiwemo chakula, dawa za meno, vinywaji, fedha na mahitaji mengine muhimu kwa niaba ya watumishi wa Wizara ya Fedha Tanzania Bara na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar, ikiwa ni sehemu ya kukamilisha tamasha la Pasaka linalofanyika kila mwaka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madereva bodaboda, bajaji wamuomba Samia kupata kadi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

VIJANA zaidi ya 67 waliopata mkopo wa pikipiki na bajaji kupitia asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma, wamemwomba Rais Samia Suluhu Hassan, kuwasaidia kupata kadi za umiliki wa vyombo hivyo.

Vijana hao wamesema wamelazimika kuomba msaada kwa Rais Samia kwa sababu ni zaidi ya mwaka sasa tangu wamalize kulipa marejesho ya mkopo huo, lakini wamekuwa wakipigwa danadana kupewa kadi za umiliki wa vyombo vyao.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na waandishi wa habari jijini hapa, wamedai kuwa tayari wameshamaliza kulipa mkopo wao tangu Februari mwaka jana lakini kupata kadi za umiliki imekuwa kikwazo kwao.

Mwenyekiti wa wanufaika wa mkopo huo, Chacha Marwa, alisema wamekuwa wakifuatilia kadi zao baada ya kumaliza malipo bila mafanikio, hivyo wanawaomba viongozi wa juu kuingilia sakata hilo.

"Mkopo tuliopata ni ule wa asilimia 10 kwa ajili ya vijana wanawake na wenye ulemavu unaotolewa na serikali, lakini kwetu tulipopata tulinunua vitendea kazi bodaboda 46 bajaji 20 na guta moja lakini sasa tumekuwa tukifuatilia kadi zetu tangu kumaliza malipo ya mkopo bila mafanikio.

"Tumekwenda Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa, Mkurugenzi lakini hakuna ambacho tumefanikiwa na viongozi wetu wa kikundi ambacho tulitumia kupata mkopo cha Umoja wa Madereva Pikipiki Mkoa wa Dodoma (UMAPIDO) wanadai kuwa sisi bado tunadaiwa Sh. milioni 71 .4 ndiyo maana hatuwezi kupata kadi zetu" alisema

Marwa, alisema kwa mujibu wa mkataba wa mkopo huo walipatiwa na kutakiwa kumaliza ndai ya miaka miwili tayari hakuna kiasai ambacho kimesalia.

"Sisi tayari tulishamaliza mkopo wetu lakini hii leo tunashangaa kuambiwa viongozi wetu wa kikundi kuwa bado tunadaiwa kiasi cha Sh. milioni 71.4, hivyo hatuwezi kupatiwa kadi zetu jambo ambalo siyo kweli na stakabadhi zetu za malipo zote zipo" alisema.

Aidha, alisema tayari wameshalipeleka suala hilo Taasisi ya Kuzua na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma na kila mwakakikundi ameshaitwa na kuhojiwa.

"TAKUKURU wametuita kila mwana kikundi na kutuhoji na kudai kuonyesha stakabadhi zetu lakini hakuna hatua ambayo imechukuliwa hadi sasa na sisi vyombo hivi bila kadi hatuwezi kufanya lolote tunamuomba Rais Samia atusaidie" alisema

Mmoja wa wanufaika hao, Irine Fred alisema hivi sasa wapo katika wakati mgumu kwani pamoja na kumaliza mkopo bado hajapatiwa kadi zao, hivyo kushindwa kufanya lolote kutokana na kukosa umiliki wa kisheria.

"Mimi mkopo huu niliupata nikiwa mjamzito lakini niliendа kununua bajaji na mimba yangu ili tuu nimalize mkopo huo na hata pale lipojifungua niliendelea kuendesha ili nimalize ndani ya mkataba. Lakini leo hii imekuwa kazi kuzipata kadi za umiliki hivyo tunaomba serikai itusaidie tuzipate" alisema.

Akitolea ufafanuzi kuhusu sakata hilo Katibu wa UMAPIDO, Remigius Fulgence, alikiri kuwa malalaimiko hayo ni ya kweli na kudai kuwa baadhi ya wanufaika wa mkopo huo bado wanadaiwa ndiyo maana hawajapata kadi zao.

Alisema: "Hawa walikopa kama kikundi lakini baaadhi yao wameshindwa kukamilisha utaratibu ndio maana wanashindwa kupata kadi zao za umiliki".

# RC atoa siku 30 kupata taarifa ya vifaa tiba katika hospitali

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, ametoa siku 30 kwa wakurugenzi wa halmashauri za mkoa huo kumpatia taarifa za vifaa tiba vilivyoletwa na Serikali kwenye hospitali za wilaya, zahanati na vituo vya afya.

Amesema lengo ni kuweka mkakati wa kuvitunza ili visiharibike haraka.

Alitoa agizo hilo juzi wilayani Ikungi katika mwendelezo wa ziara yake ya kikazi ya kukagua miradi ya maendeleo pamoja na kuzungumza na viongozi, watumishi wa umma na wakuu wa taasisi za umma.

Alisema vifaa vinavyotolewa na Serikali katika hospitali, vituo vya afya na zahanati nchini ni ghali, hivyo ni muhimu kwa watumishi kuhakikisha wanavitumia kwa ufasaha katika kutoa huduma bora kwa wananchi na kuvitunza ili viweze kudumu kwa muda mrefu.

"Haya majengo ni yetu sote wala hayajamlenga mtu yeyote ni sisi tuliokuwepo hapa na wengine ni muhimu yakalindwa na kutunzwa kwa sababu huwezi kujua siku wala saa utakapoumwa," alisema.

Kuhusu huduma za wazee, aliagiza kila halmashauri katika mkoa huo kutenga bajeti kwa ajili ya kununulia dawa za wazee kama hatua ya kuondoa malalamiko ya uduni wa utoaji wa huduma za afya katika kundi hilo.

Dendego alisema itakuwa ni jambo zuri kama maeneo yanayotoa huduma za matibabu kwa wazee yawekewe maji na chai kwa sababu wazee hao wametumikia taifa, hivyo ni muhimu wakatunzwa na kuhudumiwa vizuri.

"Tengeni fedha zinazotokana na mapato ya ndani kwa ajili ya kununua dawa za wazee kwa sababu magonjwa yao yanajulikana," alisisitiza.

Nao viongozi wa Wilaya ya Ikungi waliishukru serikali kwa kuwezesha ukamilishaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo na kumuahidi mkuu huyo wa mkoa kutekeleza maagizo aliyoyatoa, ili wananchi waweze kupata huduma bora na za uhakika karibu na maeneo yao.

Akiwa wilayani Ikungi, Dendego alifanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo ikiwemo Mradi wa Maji wa Kijiji cha Matare, Hospitali ya Wilaya ya Ikungi, Ujenzi wa Barabara ya Matongo kwa kiwango cha lami na Shule ya Mtaturu.



# Watanzania wahimizwa kumuunga mkono Samia, kudumisha amani

**Na Mwandishi Wetu**

WATANZANIA wamehimizwa kuliombea Taifa, kudumisha umoja, amani na mshikamano sambamba na kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan.

Rai hiyo imetolewa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya Puma Tanzania, Dk. Selemani Majige wakati wa hafla ya futari iliyoandaliwa na kampuni hiyo.

Futari hiyo iliongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Puma Tanzania, Fatma Abdallah, ilifanyika jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa wadau mbalimbali wakiwemo wakuu wa taasisi za umma na binafsi pamoja na wateja wa kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Akizungumza katika hafla hiyo, Dk. Majige alisema: "Tunafahamu kwa sasa tunaendelea na mfungo wa Ramadhan pamoja, hivyo wakati tukiendelea na mfungo ni vema tukaliombea Taifa letu, lakini wakati huo huo kudumisha umoja, amani na mshikamano".

Alisema kuendelea kudumisha amani kunafanya uchumi kuendelea kuimarika na biashara kwenda vizuri.

Dk. Majige alisema kulinda amani ni jambo kubwa kwani kama hakuna amani basi hata biashara haziwezi kufanyika vizuri.

Pia, aliwaomba Watanzania kuendelea kutumia mafuta ya Puma Energy Tanzania pamoja na bidhaa zake, huku akifafanua mafuta ya kampuni hiyo yana ubora na viwango vya hali ya juu.

Shekhe wa Wilaya ya Temeke, Zailai Mkoyogole, aliyemwakilisha Shekhe wa Mkoa wa Dar es Salaam, Walid Omar aliyekuwa mgeni rasmi, alisema kipindi hiki cha mwezi mtukufu wa Ramadhan jambo kubwa ni kuzidisha wema kwa maana wanadamu ni wakosaji mbele za Mungu.

Pia, alisema Mungu anapenda kuombwa, hivyo alitoa wito kwa watu wote kurejea kwa muumba kuomba msamaha.

Mkurugenzi Mkuu wa Puma Energy Tanzania, Fatma Abdallah aliwaomba Watanzania kuwaunga mkono kwa kununua bidhaa za mafuta ya kampuni hiyo.

Alisema wataendelea kuunga mkono juhudi za Serikali hasa katika kutekeleza matumizi ya nishati safi ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa lengo la kuendelea kutunza mazingira.



Mwendesha pikipiki Manispaa ya Iringa ambaye jina lake halikuweza kupatikana akiwa amepakia mshikaki raia wa kigeni watatu kama alivyokutwa eneo la RETCO barabara kuu ya Iringa -Dodoma jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Nyongeza bil.1.5/- ujenzi wa shule yamchefua RC Mtaka

**NaElizabeth John,** WANGING'OMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka amesema hajafurahishwa na ombi lililotolewa na uongozi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Usalule la nyongeza ya Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ukamilishaji wa mradi wa ujenzi wa shule hiyo.

Ombi la nyongeza za fedha hizo limekuja baada ya Sh.bilioni nne zilizotengwa awali kwa ajili ya ujenzi huo kutotosheleza.

Mtaka alitoa kauli hiyo baada ya kufanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa shule hiyo wilayani hapa.

"Sisi kwenye ngazi ya mkoa tunayo timu ya mkoa ya ufuatiliaji wa miradi na ili tujenge hoja ni lazima tujiridhishe kwamba Wanging'ombe wanaomba ziada ya Sh. bilioni 1.5 ili mradi uwe na Sh. bilioni 5.5 kutoka Sh. bilioni nne ya hapo awali," alisema Mtaka.

Mtaka alisema ni lazima kwanza mkoa ujiridhishe kwa kufuatilia katika maeneo mengine ambayo mradi kama huo umetekelezwa.

Kaimu Ofisa Elimu Mkoa wa Njombe, Leonard Msendo akiwasilisha taarifa ya timu ya ufatiliaji wa miradi ya elimu iliyofanya uchunguzi wake kwenye utekelezaji wa mradi huo ambayo ilibaini mapungufu ikiwemo mbao za ujenzi kutokuwa na ubora.

"Lakini pia milango ya madarasa inafungukia ndani na hii ni kinyume na taratibu ya majengo ya elimu, milango imefungwa wa nati za kufungia dari hivyo siyo imara," alisema Msendo.

Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Johaness Kyaruzi alisema katika mradi huo tayari madarasa 22 yamekamilika.

Alisema: "Maabara zimekamilika, nyumba za watumishi zimekamilika na mabweni mawili ya wanafunzi 80 yamekamilika".

Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Claudia Kitta alisema kupitia vikao vyao walivyokaa kuna baadhi ya mambo wamekubaliana ikiwemo miundombinu ya shule hiyo kukamilika.

# Mtoto afariki dunia kwa kuungua na jiko la mkaa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MTOTO Iyan Kingao mwenye umri wa mwaka mmoja na miezi nane mkazi wa Kata ya Kivavi katika Halmashauri ya Mji Makambako mkoani Njombe, amefariki dunia baada ya kuungua moto uliotokana na jiko la mkaa nyumbani kwao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi Mahamoud Banga aliliambia Nipashe kwamba tukio hilo lilitokea Machi 25 mwaka huu saa tatu usiku.

"Inaelezwa kwamba siku ya tukio mama wa mtoto huyo (Ana Mabiki) alitoka akiwa amemuacha mtoto akiwa amemuogesha na yupo kwenye kochi, lakini kinachoonekana kwenye zile nguo ambazo amemfunika huyo mtoto wakati anajigeuza geuza na pembeni kulikuwa na jiko la mkaa, inaonekana kuna nguo ilisogea ikagusa jiko la mkaa na kuwaka moto," alisema Kamanda Banga.

Alisema mtoto huyo alikosa msaada kwa sababu moto ulipanda na ukashika kochi na kuwaka, kwamba hadi mama yake anaporejea alikuta mtoto ameanza kuungua.

Kamanda Banga alitoa wito kwa wazazi na walezi kuwa karibu na watoto wao pamoja na kuwakagua mara kwa mara.

Awali mama mzazi wa mtoto huyo, Ana Mabiki (28) alisema alimwacha ndani mtoto wake akiwa amelala kwenye kochi na kwenda kupokea mafuta ya kupikia barabarani kwa dereva bodaboda ambaye alikuwa hakufahamu nyumbani kwake na wakati anarudi alikutana na janga hilo la moto.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Igangidung'u, Emmanuel Gadau aliwataka wazazi kuwa karibu na watoto ili kuwalinda na majanga ambayo yanaweza kuwakuta.

# W'biashara Njombe wapigwa msasa utoaji risiti elektroniki

**Na Elizabeth John,** WANGING'OMBE

WAFANYABIASHARA na wanunuzi wa bidhaa wilayani Wanging'ombe Mkoa wa Njombe, wametakiwa kutoa na kudai risiti pindi wanapofanya biashara ili kuisaidia serikali kukusanya kodi iliyo sahihi.

Akizungumza wakati wa utoaji elimu kwa mlipa kodi kwa wafanyabiashara wilayani Wanging'ombe, Ofisa Elimu kwa Mlipa Kodi TRA Mkoa wa Njombe, Brian Shoo alisema wafanyabiashara wanapaswa kuacha kufanya biashara kwa mazoea na badala yake watumie mashine za kieletroniki kutoa risiti.

"Kuna mashine hauitumii au unatoa risiti za uongo, ukikamatwa faini yake Sh.milioni 1.5 au asilimia 20 ya mauzo ya ile bidhaa uliyouza," alisema Shoo.

Ofisa Uhusiano wa TRA, Oliver Njunwa alisema kuna changamoto ya kuelewa aina ya biashara inayotakiwa kununua mashine za kieletroniki.

Baadhi ya wafanyabiashara na wakazi wa Wanging'ombe akiwemo, Belishaza Mhanga alisema elimu ya kodi ya kijiji kwa kijiji itakuwa na manufaa kwa jamii.

Hata hivyo alionya tabia ya baadhi ya maofisa wa TRA kutumia nguvu kubwa na lugha chafu wakati wa kudai kodi.

Mfanyabiashara Hamis Nurdin aliwaomba TRA kutoa mashine za kielektroniki bure kwa wafanyabiashara sambamba na matumizi teknolojia ya simu kutoa risiti.



## Mume mbaroni tuhuma kumuua mkewe

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JESHI la Polisi Mkoa wa Kusini Unguja linamshikilia, Khalfan Ali Abdallah (26) kwa tuhuma za kumuua mke wake, Zulfa Abdul Mohamed (25).

Hayo yalisemwa juzi na Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Daniel Shila, wakati akizungumza na waandishi wa habari na akisema tukio hilo lilitokea Machi 20, mwaka huu.

Wakati huohuo, alisema Jeshi la Polisi limefanikiwa kuwakamata watu watatu wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya.

Aliwataka watuhumiwa hao ni Issa Ali Kassim (36) mkazi wa Makunduchi, Muhammed Shabani Mihayo(18) mkazi wa Kibele na Hassan Khamis Abdallah (29) mkazi wa Uzi katika mkoa huo wa Kusini Unguja.

Alisema watuhumiwa hao walikamatwa na dawa za kulevya aina ya heroin kete 258 ambazo zinakadiriwa kuwa na uzito wa gramu 5.676 pamoja na bangi misokoto 38 ambazo zinauzito wa wastani wa gramu 19.

"Watuhumiwa hawa baada ya kukamatwa wamekabidhiwa kwenye Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ili kuchukuliwa hatua za kisheria" alisema Kamanda Shila.

Hata hivyo alisema kwa kipindi cha mwezi mmoja kutoka Febuari 27 hadi Machi 27 mwaka huu Jeshi la Polisi limefanikiwa kuwakamata watuhumiwa 182 katika mkoa huo kwa tuhuma za kufanya makosa mbalimbali ya uhalifu.

Aliyataja baadhi ya makosa hayo ni tuhuma za mauaji, dawa za kulevya, tuhuma za wizi wa pikipiki na makosa ya usalama barabarani.

Alisema katika makosa 214 ya barabarani kuna tukio la ajali la gari kugongana katika eneo la Unguja Ukuu na kusababisha vifo vya watu watatu ambao ni raia wa kigeni.

Aidha, alisema hali ya ulinzi na usalama katika mkoa huo imeimarishwa katika kipindi chote hasa wakati ambapo waumini wa dini ya kikristo wanasherehekea Sikukuu ya Pasaka.

# Mariam Mwinyi ataka mwongozo katika utoaji wa elimu ya hedhi

**Na Mwandishi Wetu**

MKE wa Rais wa Zanzibar, Mariam Mwinyi ameitaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amani kuandaa mwongozo wa utoaji elimu ya hedhi kwa shule za msingi na sekondari.

Mariam ambaye pia ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation, alitoa rai hiyo juzi wakati wa hafla ya ugawaji taulo za kike kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi na Sekondari Jadida iliyopo Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Mariam alisema kuna umuhimu wa kuwepo muongozo wa elimu ya hedhi salama kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari visiwani Zanziabar.

Alisema wanafunzi wa kike wanapitia wakati mgumu kwa kukosa baadhi ya vipindi vya masomo na kuchangia kushuka wa viwango vya ufaulu wanapokuwa kwenye kipindi cha hedhi.

Alieleza kuwa suala la hedhi salama ni changamoto kutokana na kukosekana kwa uelewa sahihi kwa watoto wa kike na jamii, hivyo ni vyema kwa Wizara ya Elimu kuwa na mikakati itakayosaidia kuongeza uelewa.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Leila Muhammed Mussa alisema, serikali inazingatia suala la hedhi salama kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Hata hivyo alisema pamoja na juhudi zinazochukuliwa kuna changamoto ya uelewa mdogo kwa jamii hasa kwa baadhi ya wazazi kushindwa kuwaeleza watoto wao njia salama za kujihifadhi wanapokuwa kwenye kipindi hicho.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation, Fatma Fungo, alisema ugawaji wa taulo hizo kwa wanafunzi wa kike utawasaidia kupunguza usumbufu wanaopitia wanapokuwa kwenye mizunguko ya hedhi.

Alisema taulo hizo zitawasaidia wanafunzi wa kike kuwa kwenye hedhi salama na kuwezesha kutimiza ndoto zao hasa kushiriki kikamilifu masomo wanapokuwa kwenye siku zao.

Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation (ZMBF), mbali na shughuli nyingi zinazofanywa na taasisi hiyo, ikiwemo kupiga vita udhalilishaji, masuala ya wanawake, vijana na watoto pia inaendeleza kampeni yake ya "Mariam Mwinyi Walkathon".

Kampeni hiyo yenye lengo la kuimarisha afya za wananchi na kutekeleza mikakati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia kampeni ya 'afya bora', inayowafikishia huduma bora za matibabu wananchi.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Unguja Gaudianus Kamugisha akitoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu hali ya kiusalama katika mkoa huo jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# THBUB: Kuna migogoro mingi ya ardhi wananchi, JWTZ

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imesema kuna migogoro mingi ya ardhi ambayo inahusisha wananchi na Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ).

Imesema hali hiyo inaweza kuleta mtafaruku baina ya pande mbili hizo endapo hatua za haraka zisipochukuliwa.

Kamishna wa Tume hiyo Zanzibar, Khatib Mwinyichande, aliyasema hayo visiwani hapa mwishoni mwa wiki, wakati akitoa taarifa ya chunguzi maalum zilizofanywa na tume hiyo kati ya Machi hadi Mei 2022 na Machi hadi Juni mwaka 2023.

Kamisha huyo aliitaka Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, kushirikiana na JWTZ, kuitafutia ufumbuzi migogoro ya ardhi isiyo ya lazima.

Aidha alisema tume hiyo ilifanya uchunguzi kuhusu madai ya wananchi wa Kidimni Paris Wilaya ya Kati Unguja kuhusu kuvunjiwa nyumba zao na kuhamishwa kwa nguvu na wanajeshi wa Kambi 11KJ iliyopo Ubago.

Alisema kuwa katika lalamiko hilo wananchi wa Kidimni walidai Juni mwaka 2022 askari wa JWTZ walifika katika maeneo yao na kuvunja nyumba bila ya kutoa taarifa za awali.

Kamishna huyo alisema kitendo hicho kilisababisha baadhi yao kufariki kutokana na mshituko, kuharibika na kupoteza mali zao, kukosa mahali pa kuishi na watoto kukosa haki yao ya msingi ya kupata elimu.

Hata hivyo, alisema katika uchunguzi huo tume ilibaini kuwa nyumba zilizokuwepo katika eneo hilo zilivunjwa na askari wa JWTZ na kubaini kulikuwa na ahadi ya wananchi kulipwa fidia.

Alisema kuwa uchunguzi pia umebaini jeshi hilo halikutoa taarifa ya kuvunja nyumba kwa walalamikaji ili waweze kuhamisha mali zao kama inavyoeleza sheria.

Hivyo aliishauri Wizara ya Ardhi kuendelea kushirikiana na JWTZ na Wizara ya Fedha ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, kuhakikisha wananchi waliovunjiwa nyumba na vibanda katika eneo hilo wanalipwa fidia kama walivyokubaliana.

Pia aliitaka wizara hiyo ihakikishe kamati iliyoundwa na serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kupitia maeneo ya kambi za JWTZ hususani zenye migogoro kwa ajili ya kutafuta ufumbuzi kutoa taarifa yake.

Alisema kuwa kamati hiyo pia iwasilishe Wizara ya Ardhi ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Ardhi Zanzibar kwa ajili ya kutekeleza mapendekezo yaliyokuwepo katika taarifa hiyo ili kuepusha athari zaidi.

Katibu Msaidizi wa Tume hiyo, Juma Msafiri Karibona, alisema wakati wa uchunguzi wao walibaini kuna hoja ya migogoro baina ya wananchi na kambi za jeshi.

# Kilio cha huduma dhidi ya hatari fedha kupotea

**Na Mwandishi Wetu**

KUNA sura kuu mbili zinazokinzana katika mwenendo wa bajeti ya mapato na matumizi kiserikali; ufinyu wa fedha zinazohitajika kutimiza mahitaji ya mipango ya kijamii, huku upande wa pili kuna kutoweka fedha hizo katika mazingira tata.

Hapo inajenga tafsiri namna utolewaji huduma muhimu za kijamii unavyokwazwa, katika nafasi ya kipekee ikigusa sekta za afya na elimu, ambazo zimeshika maisha ya kila siku - asubuhi hadi jioni na mahitaji yake hayakwepeki.

Hata ikirejewa katika uchambuzi wa ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka wa Fedha 2021/22, uliofanywa na Taasisi ya WAJIBU, imebainishwa miamala mbalimbali yenye viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu wa fedha za umma.

Katika uchambuzi wake, taasisi hiyo imebaini kwamba kiasi ambacho aidha hakikukusanywa au kimetumiwa na serikali pasi na kupata tija yoyote (nugatory expenditure) kimepungua kwa asilimia 33 kutoka Sh. bilioni 4,590.73 kwa mwaka wa fedha 2020/21 hadi Sh. bilioni 3,084.55 kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Vilevile, uchambuzi umebaini kuwa mashirika ya umma yamekuwa na ongezeko la asilimia 43 ya jumla ya miamala ambayo ina viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu kutoka Sh. bilioni 1,408.36 mwaka wa fedha 2020/21, hadi Sh. bilioni 2,015.78 mwaka wa fedha 2021/22.

Hii ina maana kwamba jumla ya miamala yenye viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu katika mashirika ya umma pekee ni Sh. bilioni 2,015.78 sawa na asilimia 65 ya jumla ya miamala yote yenye viashiria vya rushwa ubadhirifu na udanganyifu ya Sh. bilioni 3,084.55 kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Kwa ujumla, katika uchambuzi wake huo, taasisi hiyo imebainisha miamala mbalimbali yenye viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu wa fedha za umma, ikisababisha hatari ya upotevu wa Sh. bilioni 1,770.84 mwaka 2019/20, Sh. bilioni 4,590.73 mwaka 2020/21 na Sh. bilioni 3,084.55 mwaka 2021/22.

Hii ina maana kwamba, jumla ya Sh. trilioni 9.446 ziko hatarini kupotea katika mazingira yenye viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu katika miaka mitatu ya fedha (2019/20-2021/22).

Jedwali la mwenendo wa viasharia vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu kwa kipindi cha miaka mitatu

| Taasisi | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|---|
| Serikali Kuu | Bil 560.19/- | Bil 1,781.77 | Bil 770.91/- |
| S/Mitaa | Bil 863.85/- | Bil 1,400.6/- | Bil 297.86/- |
| Mashirika | Bil 346.8/- | Bil 1,408.36 | Bil. 2,015.78 |
| **Jumla** | Bil 1,770.84/- | Bil 4,590.73/- | Bil 3,084,55/- |

***CHANZO:*** Ripoti ya Uwajibikaji - Viashiria vya Rushwa, Udanganyifu na Ubadhirifu 2021/22 ya Taasisi ya WAJIBU



Waziri Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohammed Mchengerwa. **PICHA: MTANDAO**

> Hii ina maana kwamba, jumla ya Sh. trilioni 9.446 ziko hatarini kupotea katika mazingira yenye viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu katika miaka mitatu ya fedha (2019/20-2021/22).

### SEKTA YA ELIMU

Kiasi hicho kama kingelielekezwa kutatua uhaba wa miundombinu shuleni, kingelitosha kujenga vyumba vya madarasa mpya 472,306 au matundu milioni 8.587 ya vyoo.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), chumba kimoja cha darasa kinajengwa kwa Sh. milioni 20 kikiwa na samani zake zote huku tundu moja la choo likijengwa kwa Sh. milioni 1.1.

Katika ripoti yake ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Mwaka 2021/22 iliyowasilishwa bungeni Aprili 6, mwaka jana, CAG Kichere anaeleza kuwa tathmini yake kuhusu miundombinu ya shule za msingi za halmashauri 45 alizozikagua, ilibaini zilikuwa na upungufu wa madarasa 27,316, madawati 158,066, vyoo 56,530 kwa ajili ya wanafunzi na nyumba za walimu 35,684.

Jedwali la uhaba wa miundombinu ya shule za msingi.

| Miundombinu | Mahitaji | Yaliyopo | Upungufu |
|---|---|---|---|
| Madawati | 596,872 | 438,806 | 158,066 |
| Vyoo (funzi) | 100,630 | 44,100 | 56,530 |
| Nyumba wal | 45,557 | 9,873 | 35,684 |
| Viti na meza | 63,764 | 33,935 | 29,829 |
| Madarasa | 57,866 | 30,550 | 27,316 |
| Ofisi walimu | 4,997 | 2,731 | 2,266 |
| Vyoo walimu | 1,520 | 898 | 622 |
| **JUMLA** | 871,206 | 560,893 | 310,313 |

***CHANZO:*** Ripoti ya CAG, Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa 2021/22 (Uk. 116).



### SEKTA YA AFYA

Sh. trilioni 9.446 zilizo hatarini kupotea katika mazingira tajwa hapo juu, kama kingeelekezwa kwenye sekta ya afya, kingetosha kujenga hospitali 1,246 za wilaya au vituo vya afya 8,056 au zahanati 31,419.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, ujenzi wa zahanati unagharimu wastani wa Sh. 300,641,028 (vifaa vinagharimu Sh. 87,677,593.70); ujenzi wa kituo cha afya unagharimu wastani wa Sh. 1,172,583477 kikiwa na majengo 11 (vifaa vinagharimu Sh. 501,728550) huku ujenzi wa hospitali ya wilaya ukigharimu Sh. bilioni 5.781 (vifaa vinagharimu Sh. bilioni 3.4).

Kimsingi, kuwapo hatari ya upotevu wa fedha za umma iliyoibuliwa na CAG ilhali nchi inakabiliwa na uhaba wa miundombuni na samani shuleni, kunakwaza utekelezaji Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26).

Mpango huo umebainisha malengo muhimu katika sekta ya elimu yanayotakiwa kufikiwa ifikapo mwaka 2026, ambayo ni pamoja na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi na sekondari kama vile ujenzi wa vyumba vya madarasa, ununuzi wa madawati na vitabu, kuboresha uwiano wa vyoo na mazingira ya kazi kwa walimu katika ngazi zote, malipo yao na makazi kuwa karibu na maeneo ya kazi.

Hatari hiyo ya upotevu wa mabilioni ya shilingi ilhali nchi inakabiliwa na uhaba wa vituo vya kutolea huduma za afya, unakwaza utekelezaji Sera ya Afya (2007), Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020-2025 na Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) wa mwaka 2008. Vyote hivyo vinaoelekeza serikali kuhakikisha kunakuwa na zahanati kila kijiji, kituo cha afya kila kata na hospitali kwa kila wilaya nchini.

## Russia yaitaka Ukraine kuikabidhi washukiwa wa ugaidi

**MOSCOW,** Russia

RUSSIA imeitaka Ukraine kuikabidhi watu kadhaa kutoka nchini humo, akiwemo mkuu wake wa idara ya usalama, Vasyl Maliuk kwa madai kuwa walihusika na vitendo vya kigaidi katika ardhi ya Russia.

Katika taarifa iliyotoa jana, Wizara ya Mambo ya Nje ya Russia ilirudia madai kwamba Ukraine ilihusika katika shambulizi lililofanywa Machi 22 dhidi ya ukumbi mmoja wa tamasha nje ya Moscow na pia kuishtumu kwa mashambulizi kadhaa na mauaji yaliyofanyika ndani ya nchi hiyo.

Ikitaja mikataba miwili ya kimataifa ya kupambana na ugaidi, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Russia iliitaka Ukraine kutimiza ombi hilo, kwa kuzingatia miongozo ya mikataba hiyo.

Taarifa hiyo ilisema kuwa Maliuk alikiri kupanga ulipuaji wa daraja la Crimea Oktoba 2022 na kufichua habari za idara yake kuhusu mashambulizi mengine ya kigaidi.

Hata hivyo, Shirika la ujasusi la Ukraine, (SBU), lilisema taarifa hizo kuhusu ugaidi kutoka kwa taifa ililoliita la kigaidi, hazina msingi wowote.

Katika hatua nyingine Russia imeendelea kufanya operesheni za kupambana na ugaidi huko Dagestan baada ya shambulio ambalo lilichukua uhai wa watu wasiopungua 144.

Kamati ya Taifa inayoshughulikia ugaidi, ilisema Russia inafanya operesheni za kupambana na ugaidi katika mkoa wa kusini wa Dagestan, na kuwatia mbaroni watu wengine watatu.

Aidha, ilielezwa kuwa taifa hilo liko katika hali ya tahadhari ya kiwango cha juu kutokana na shambulizi hilo baya zaidi kuwahi kutokea nchini humo katika kipindi cha miaka 20.

Kamati hiyo ilisema idara za usalama ziliwakamata majambazi watatu ambao walikuwa wakipanga matukio kadhaa ya kigaidi, na kwamba wakati wa ukaguzi wa maeneo ambayo wahalifu hao walikamatwa, zilipatikana bunduki za rashasha, risasi, na vifaa vya milipuko ambavyo vilikuwa tayari kutumiwa.

Awali, kamati hiyo ilisema washukiwa wa uhalifu walizuiliwa na idara za usalama katika nyumba kadhaa kwenye maeneo ya makazi ya mji mkuu wa mkoa Makhachkala na moja ya miji mikubwa katika Jamhuri ya Kaspiysk. **DW, VOA**

# Uhuru warejea katika hospitali ya Al-Shifa Gaza

**GAZA,** Palestina

UHURU umerejea katika hospitali ya Al-Shifa huko Ukanda wa Gaza baada ya vikosi vya Jeshi la Israel kujiondoa katika jengo la hospitali hiyo ambalo liliwekwa kizuizini kwa takribani siku 14.

Kulingana na taarifa ya Jeshi la Ulinzi la Israel iliyotolewa jana, hatua hiyo imejiri baada ya kukamilisha shughuli mahususi za operesheni za kudhibiti mikakati ya kundi la Hamas katika eneo la hospitali hiyo.

"Wanajeshi waliwaua magaidi katika mapigano ya karibu, walipata silaha nyingi na hati za kijasusi katika hospitali nzima, huku wakizuia madhara kwa raia, wagonjwa na timu za matibabu," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

**Pia alibainisha kuwa zaidi ya watu 30 waliojeruhiwa walisafirishwa kutoka Al-Shifa hadi Hospitali ya Al-Ahli Baptist mashariki mwa Jiji la Gaza.**

Msemaji wa Ulinzi wa Raia wa Gaza, Kapteni Mahmoud Bassal, kwenye eneo la tukio aliiambia CNN kwamba hospitali hiyo, ambayo ilikuwa kituo kikuu cha matibabu katika eneo hilo, imeharibiwa kabisa na kuchomwa moto.

"Miili ya waliojeruhiwa na waliokufa inajaza uwanja wa hospitali. Pia kuna miili iliyozikwa katika yadi za hospitali," alisema Kapteni Bassal.

Pia alibainisha kuwa zaidi ya watu 30 waliojeruhiwa walisafirishwa kutoka Al-Shifa hadi Hospitali ya Al-Ahli Baptist mashariki mwa Jiji la Gaza.

Aidha, picha mbalimbli zilizochapishwa kwenye mitandao ya kijamii kutoka eneo hilo zilionyesha uharibifu mkubwa na majengo yaliyochomwa moto ndani ya jengo la hospitali hiyo.

Wanajeshi wa Israel walivamia hospitali ya Al-Shifa kwa mara ya kwanza mwezi Novemba, 2023, na kwamba operesheni yake ya pili ya kijeshi iliyofuata licha ya kusema ilikuwa imekamilisha kuvunja muundo wa amri ya Hamas kaskazini mwa Gaza.

Jeshi hilo lilisema raia, wagonjwa, na timu za matibabu walihamishwa wakati wa operesheni ingawa Wapalestina ndani na karibu na Al-Shifa waliripoti majeruhi na kukamatwa kwa wananchi. **CNN**



Miguu ya baadhi ya wananchi wa Libya ikikanyaga picha ya Waziri Mkuu wa Taifa hilo, Abdulhamid Al-Dbeibah, ambaye makazi yake yalishambuliwa jana kwa makombora yanayorushwa kwa roketi. **PICHA: MTANDAO**

# Makazi ya Al-Dbeibah yashambuliwa

**TRIPOLI,** Libya

WAZIRI mmoja wa nchini Libya amebainisha kuwa makazi ya Waziri Mkuu wa taifa hilo, Abdulhamid Al-Dbeibah yameshambuliwa kwa makombora ya kurushwa na roketi, shambulio ambalo halikusababisha majeruhi.

Akizungumza na shirika la habari la Routers jana kwa sharti la kutokutajwa jina, alisema shambulio hilo mbali na kutokusababisha madhara kwa binadamu lakini lilisababisha uharibifu wa miundombinu.

Wakizungumzia tukio hilo wananchi wawili walisema walisikia milipuko mikubwa karibu na bahari katika kitongoji cha kifahari cha Hay Andalus cha mjini Tripoli, ambako ni makazi ya Waziri Mkuu Dbeibah.

Mwingine alisema baada ya milipuko hiyo mikubwa kusikika, walishuhudia maofisa wengi wa usalama na magari yao wakipelekwa karibu na eneo hilo.

Hata hivyo, Libya haijapata amani au utulivu tangu uasi wa 2011 uliongwa mkono na Jumuiya ya Kujihami ya (NATO), na iligawanyika mwaka 2014 kati ya pande za mashariki na magharibi, na tawala hasimu zikiongoza kila upande.

Vile vile, serikali ya umoja wa taifa ya Dbeibah iliundwa kupitia mchakato ulioungwa mkono na Umoja wa Mataifa (UN) mwaka 2021 lakini bunge huko mashariki, lilipinga kutambua uhalali wa serikali hiyo mwishoni mwa mwaka baada ya jaribio ambalo halikufanikiwa la kuandaa uchaguzi wa taifa, hali ambayo ilisababisha mzozo wa kisiasa wa muda mrefu.

Mapema mwezi Machi, viongozi watatu wakuu walisema walikubaliana juu ya umuhimu wa kuunda serikali mpya ya umoja ambayo itasimamia uchaguzi uliocheleweshwa kwa muda mrefu.

Dbeibah aliapa kuwa hatokabidhi madaraka kwa serikali mpya bila uchaguzi wa taifa kufanyika. **VOA**

# KOCHA KENGOLD FC AWAONYA WACHEZAJI MBIO CHAMPIONSHIP

**Na Saada Akida**

HUKU wakiwa kileleni katika msimamo wa Ligi ya Championship, Kocha wa KenGold, Jumanne Challe, amewataka wachezaji wake kutoridhika, badala yake kuzisaka pointi 12 katika michezo minne iliyosalia ya ligi hiyo.

Mwishoni mwa wiki KenGold wakibanwa mbavu kwa kulazimishwa sare ya mabao 3-3 dhidi ya Mbuni FC, hata hivyo matokeo hayo hayakuweza kuwapndoa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ambayo mshindi wa kwanza na wapili anapanda moja kwa moja Ligi Kuu Bara.

KenGold wanaongoza msimamo wa ligi hiyo wakiwa na pointi 61, wakifuatiwa na Pamba wenye pointi 58 na Mbeya Kwanza wakishika nafasi ya tatu na pointi zao 56, wakati huu zikisalia mechi nne ligi hiyo kutamatikika.

**Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Challe, alisema michezo ya mwisho wa msimu imekuwa na changamoto sana, hivyo kunahitajika umakini sana kumaliza msimu wakiwa mabingwa na kutimiza malengo yao.**

Alisema wanatakiwa kuwa makini na kupambana katika kila hatua kuhakikisha wanafanikiwa kuvuna alama zote 12 za michezo minne kwa sababu wakipoteza na waliopo chini yao wakishinda watakuwa wamepoteza malengo yao.

"Bado tuna kazi ya kufanya, tunamaliza msimu kama tulivyopanga, lakini tuweze kutimiza malengo yetu, tunahitaji kushinda kila mchezo ulio mbele yetu bila kuangalia matokeo ya wale wanaotufuatia.

"Haya yatafanikiwa iwapo wachezaji watakuwa tayari kuipambania timu, kitu ambacho kimekuwa kikionyeshwa na vijana wangu tangu mwanzoni mwa msimu na tukiwa na mwendelezo huo michezo iliyosalia basi tutaenda kutimiza malengo yetu," alisema.

Aliongeza kuwa mechi za mzunguko wa pili zimekuwa za ushindani kutokana na kila timu kuhitaji kushinda, ili ziweze kutimiza malengo yao, na kwamba licha ya kuwa kileleni zaidi ya alama nne kutoka kwa anayeshika nafasi ya pili, hawapaswi kubweteka.

"Pointi nne ni ndogo sana katika soka kwa sababu ukipoteza mechi moja na sare moja na aliyekuwa chini yetu akishinda mechi mbili basi tutakuwa tumepoteza malengo yetu ya kumaliza msimu tukiwa kileleni," alisema kocha huyo.

KIKAPU...



Vijana wakiwania mpira wakati wakifanya mazoezi ya mpira wa Kikapu katika viwanja vya Kituo cha Michezo cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mapinduzi yaiiua Kasulu United 9-0 Ligi Daraja la Pili

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mapinduzi FC imeendelea kujichimbia kileleni mwa msimamo wa Ligi Daraja la Pili, 'First League', ikisaka nafasi ya kupanda Ligi ya Championship, baada ya kuisulubu bila huruma Kasulu United mabao 9-0 katika mechi iliyochezwa juzi, Uwanja wa Lake Tanganyika Kigoma.

Ikiwa mbele ya mashabiki wao, Kasulu United ilishindwa kabisa kuzuia mafuriko ya mabao, na kujikuta ikibugizwa idadi hiyo kubwa ya mabao na kuifanya kuendelea kuburuza mkia kwenye Kundi B, ikiwa na pointi moja tu mpaka sasa katika mechi 14 ilizocheza.

Matokeo hayo yanaifanya Mapinduzi kuongoza kundi hilo ikiwa na pointi 28.

Timu ya Tanesco nayo ikiwa ugenini, Uwanja wa Kambarage Shinyanga, ilitoa kipigo cha mabao 6-2 dhidi ya wenyeji wao, Kurugenzi katika mfululizo wa mechi za ligi hiyo inayoelekea ukingoni.

Matokeo hayo yanaifanya Tanesco kukaa kwenye nafasi ya tatu ya msimamo wa ligi hiyo, ikifikisha pointi 27 kwenye Kundi B, nayo pia ikiwa katika nafasi nzuri ya kutinga nane bora ya ligi hiyo.

Katika michezo mingine ya Kundi B, Rhino Rangers iliiadhibu TRA mabao 3-0, mechi ikichezwa Shule ya Sekondari Tabora, na Mwadui ikaisasambua Alliance FC mabao 4-1 kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari Nyankumbu, Geita.

Katika mechi za Kundi A zilizochezwa juzi, African Sports ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya African Lyon, Mkwakwani Tanga, Dar City ikaichapa Malimao bao 1-0, Uwanja wa Manungu Complex, Turiani Morogoro, na Kiluvya ikatoka suluhu dhidi ya Tunduru Korosho, Uwanja wa Mabatini, Mlandizi, Pwani.

# *JKU yajiona robo fainali Kombe la FA Zanzibar*

**Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

HAKUNA kukata tamaa, ndivyo anavyosema Kocha Mkuu wa JKU SC, Salum Ali Haji, baada ya kuweka bayana kuwa bado anamatumaini makubwa ya kutetea ubingwa wao wa michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka la Zanzibar (ZFF), maarufu FA Cup.

JKU SC katika hatua hii ya 16-bora itashuka dimbani kuumana na Nyangobo FC kutoka Ligi ya Mkoa wa Mjini Magharibi.

Michuano hiyo ya FA katika hatua ya 16-bora imepangwa kuchezwa kuanzia Aprili 18 hadi 21, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Haji, alisema haoni kikwazo kwa timu yake kushindwa kusonga mbele katika micbuano hii hasa mchezo wao wa hatua ya 16-bora.

Alisema kukutana na timu kutoka Ligi ya Mkoa wa Mjini Magharibi kwao wao ni njia nyeupe kusonga mbele katika hatua ya robo fainali ya michuano hiyo ingawa pia umakini unahitajika.

Alisema mpango wao mkubwa upo katika kuhakikisha wanatetea taji lao la michuano hiyo ya FA ili kuweka rekodi ndani ya timu yao kufanya hivyo mara mbili mfululizo.

"Hatuwahofii sana wapinzani wetu katika hatua hii ya 16-bora kwakuwa tuna kikosi ambacho kitaweza kupata matokeo tu kwa timu hii ambayo tunacheza nayo, mahehsabu yetu tunaangalia zaidi hatua ya robo fainali,"alisema.

JKU imeanza mazoezi tangu juzi, Jumapili baada ya kumpumzika takriban wiki tatu kwa ajili ya kupisha ibada ya funga ya Mwezi wa Ramadhani inayoendelea.

Hata hivyo, aliwaomba mashabiki wao kuendelea kuipa hamasa timu hiyo kama ilivyokuwa mwanzo wa msimu ili ifanikiwe mipango yake iliyojiwekea ya kuvuna mataji msimu huu.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### NEVES AGOMBEWA EPL

LIVERPOOL imeungana na Manchester United na Chelsea katika mbio za kumsajili kiungo wa kati wa Benfica na Ureno, Joao Neves mwenye umri wa miaka 19, ambaye ana kipengele cha kutolewa cha euro milioni 120. ***(O Jogo, via Sport Witness)***

### FRIMPONG AVUTIA VIGOGO

MANCHESTER United na Manchester City zinavutiwa na beki wa Bayer Leverkusen, Jeremie Frimpong, 23. ***(Sun)***

### PAQUETA AWANIWA CITY

KLABU ya Manchester City inatazamia kufufua upya azma yao ya kumnunua kiungo wa kati wa West Ham na Brazil, Lucas Paqueta, 26. ***(Football Insider)***

### PHILLIPS AWANIWA LEEDS

LEEDS United inapania kumsajili tena kiungo wa kati wa England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 28, kwa takribani pauni milioni 30 kutoka Manchester City msimu huu wa majira ya joto. ***(Sun)***

### ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United itaongeza juhudi za kumsajili mchezaji wa safu ya ulinzi msimu huu na kumpa mlinzi, Paul Dummett mwenye umri wa miaka 32, mkataba mpya baada ya nahodha Jamaal Lascelles kuwa nje ya dimba hadi miezi tisa kutokana na jeraha la goti. ***(Newcastle Chronicle)***

### HECKINGBOTTOM, SUNDERLAND

KOCHA wa zamani wa Sheffield United, Paul Heckingbottom anaongoza orodha ya wanaotarajiwa kuinoa Sunderland. ***(Sun)***

### RAPHINHA ANOGEWA BARCA

BARCELONA ipo tayari kupokea ofa ya kumuuza Raphinha, 27, msimu huu wa majira ya joto ili kupunguza wasiwasi wa kifedha, lakini mshambuliaji huyo wa Brazil hataki kuondoka. ***(Sport)***

### VELIZ KWA MKOPO

KLABU ya Tottenham Hotspur inapanga kumtoa kwa mkopo Alejo Veliz, 20, kwa klabu tofauti msimu ujao kwani wanahisi mshambuliaji huyo wa Argentina wa Chini ya miaka 20, hajacheza mechi za kutosha katika kipindi chake cha sasa akiwa na Sevilla. ***(Fabrizio Romano)***

### AMORIM KUFANYA UAMUZI

KOCHA wa Sporting Lisbon, Ruben Amorim, angependelea kujiunga na Liverpool iwapo atapewa kazi hiyo, lakini atafanya uamuzi kuhusu mustakabali wake mwishoni mwa msimu huu. ***(Correio da Manha)***

### GRAY ANYATIWA SPURS

KLABU ya Tottenham imejiunga na mbio za kumsajili kiungo wa kati wa Leeds United mwenye umri wa miaka 18, Archie Gray, huku Liverpool pia ikimnyatia mchezaji huyo wa Kimataifa wa England chini ya miaka 21. ***(Football Insider)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA



# GUARDIOLA: UBINGWA EPL HAUPO MIKONONI MWETU

**Ni Liverpool, yeyote aliye wa kwanza anapendekezwa, wa pili ni Arsenal na sisi ni...**

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesema Manchester City sasa ni ya tatu kati ya timu zinazoweza kushinda taji la Ligi Kuu England baada ya suluhu na Arsenal kwenye Uwanja wa Etihad, Jumapili.

**Matokeo hayo yanaifanya City kuwa nafasi ya tatu kwenye msimamo, pointi moja nyuma ya Arsenal katika nafasi ya pili na alama tatu nyuma ya vinara, Liverpool.**

Huku kukiwa na mechi tisa, taji hilo halipo mikononi mwao na Guardiola alisema timu yake sasa iko chini ya kutwaa taji hilo kwa msimu wa nne mfululizo.

Alipoulizwa kama Liverpool sasa ndio wenye nafasi kubwa ya kushinda taji hilo, Guardiola alisema: "Ndiyo. Yeyote aliye wa kwanza anapendekezwa, wa pili ni Arsenal na sisi ni wa tatu.

"Haupo mikononi mwetu - tunachoweza kufanya ni kufikiria mchezo unaofuata dhidi ya Aston Villa. Ikiwa uko kinara wa ligi, kama tulivyokuwa hapo awali, wewe una nafasi kubwa.

City walitawala muda mwingi wa mchezo dhidi ya Arsenal, lakini waliweza kupiga shuti moja pekee lililolenga lango.

Ilikuwa ni mara ya kwanza kushindwa kufunga katika mchezo wa ligi kwenye Uwanja wa Etihad tangu Oktoba 2021, na baadaye Guardiola alitania kwamba kulikuwa na njia moja tu ya kupita safu ya ulinzi ya Arsenal.

"Ua mtu," alisema. "Cheza na tisa. Wanalinda vizuri na sana, wakimzunguka Erling Haaland. Walilinda vema na watu wengi. Kuna njia tofauti."

Naye Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, alisema: "Unataka kushinda mchezo, unajitayarisha kushinda, lakini ikiwa huwezi kushinda, hakikisha unatoka sare."

"Tulifanya hivyo. Miezi 11 iliyopita tulikuwa hapa na hadithi ilikuwa tofauti sana. Mnapaswa kupiga hatua kama timu na leo tumefanya hivyo. Bado tuna mengi zaidi yanakuja.

"Inakuonesha kujituma kwa kila mchezaji, nidhamu waliyoonesha na jinsi wanavyoshindana. Kitu kimoja ni kucheza mechi ya mpira na kingine ni kushindana ndani yake, leo tulifanya hivyo vizuri."

Timu zote mbili bado ziko hai katika Ligi ya Mabingwa Ulaya, Arsenal itacheza na Bayern Munich na Man City itaivaa Real Madrid katika robo fainali Jumanne ya wiki ijayo.

Kabla ya hapo, Man City watawakaribisha Aston Villa nao Arsenal watacheza na Luton Town huko Emirates Jumatano hii katika mechi ya Ligi Kuu ya England.



# KLOPP AKUNWA NA BAO LA SALAH

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amesema Mohamed Salah alitekeleza jukumu lake muhimu kwa Liverpool baada ya fowadi huyo kufunga wakati wa ushindi wa mabao 2-1 wa Ligi Kuu England dhidi ya Brighton kwenye Uwanja wa Anfield Jumapili.

Bao la Salah kipindi cha pili akiunganisha pasi ya Alexis Mac Allister, lilikamilisha mechi ya Liverpool baada ya Luis Diaz mapema kufuta bao la kuongoza la Danny Welbeck kwa timu ya Roberto De Zerbi.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Misri, amepoteza nafasi nyingi zaidi katika mechi ya Ligi Kuu tangu Zlatan Ibrahimovic kukosa nafasi 12 alipokuwa akichezea Manchester United dhidi ya Burnley Oktoba 2016.

Na Kocha wa Liverpool, Klopp alimpongeza Salah kwa uwezo wa kufunga bao la ushindi la timu hiyo.

"Nadhani Mo Salah angemaliza hali zote hizo katika taaluma yake, lakini hiyo ingekuwa namba ya kichaa," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari baada ya mechi.

"Ulikuwa mpira wa ajabu kutoka kwa Dominik Szoboszlai. Ni ubunifu na ubora, kuona hivyo. Anamwona Macca Mac Allister na mguso wake wa kwanza ni wa ajabu na kisha anamuona Mo.

"Jinsi tulivyopoteza wakati mwingine wote, ilikuwa nzuri tulikuwa na wakati huu wa mpira wa miguu kumaliza mchezo."

Licha ya kuwa nyuma kwa bao la kwanza la Welbeck, Liverpool waliepuka kuanguka katika mbio za ubingwa kwa kuwa na ujasiri wa kusawazisha na kisha kushinda mchezo huo.

Klopp alisema timu yake na mashabiki wa klabu hiyo hawana wasiwasi kama walivyokuwa wakati wa changamoto za ubingwa uliopita.

"Katika suala la kuwa na wasiwasi kama, tulikuwa na wasiwasi zaidi miaka iliyopita," Klopp alisema.

"Tungekuwa mbele kwa bao 1-0 na hakuna mtu ambaye angetulia hadi ipite tatu au nne bila."

# Rodrygo aipeleka Madrid karibu na kutwaa ubingwa



**MADRID,** Hispania

RODYGO alifunga bao katika kila kipindi wakati Real Madrid ikipata ushindi wa mabao 2-0 nyumbani dhidi ya Athletic Bilbao Jumapili, na hivyo kujikita kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.

Madrid ina pointi 75, nane mbele ya Barcelona katika nafasi ya pili na 10 mbele ya Girona iliyopo nafasi ya tatu. Bilbao wapo nafasi ya nne wakiwa na pointi 56.

"Ni siku maalum. Kufunga bao ukivaa jezi hii daima ni muhimu," alisema Rodrygo baada ya mchezo huo. "Nimefurahishwa na ushindi.

"Bao la kwanza ni hatua ninayopenda kufanya sana. Ninapenda kuingia ndani na kupiga mashuti. Nataka kufunga mabao mengi zaidi kama hayo. Sasa katika hatua hii ya mwisho ya msimu wa LaLiga lazima tupate pointi ili kukaribia kushinda kombe hili."

Matokeo hayo yamegonga matumaini ya Bilbao walio katika nafasi ya nne ya kupata nafasi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao kwani wako pointi moja pekee mbele ya Atletico Madrid, ambao jana Jumatatu walicheza dhidi ya Villarreal.

Rodrygo alifunga bao baada ya dakika nane, akiupinda mpira kwa utulivu hadi kona ya mbali baada ya kukimbia kwa kasi hadi kwenye ukingo wa eneo la goli kutoka upande wa kushoto.

"Unaweza kusema anajisikia vizuri akiwa upande wa kushoto, lakini yuko vizuri kila mahali," alisema kocha wa Madrid, Carlo Ancelotti, baada ya mchezo huo.

"Tusisahau alifunga mabao mawili akicheza upande wa kulia kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya."

# Lewandowski aikataa Saudia

**BARCELONA,** Hispania

MSHAMBULIAJI nyota wa Barcelona, Robert Lewandowski, amekataa mkataba mnono nchini Saudi Arabia ili kubakia Barcelona, kwa mujibu wa ripoti kutoka Hispania.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Poland alijiunga na Barca katika dirisha la usajili la kiangazi la 2022 na akaiwezesha klabu hiyo kutwaa taji lao la kwanza la LaLiga katika kipindi cha miaka minne katika msimu wake wa kwanza, akifunga mabao 23 kwenye ligi na 33 katika mashindano yote.

Msimu wa pili wa Lewandowski katika klabu hiyo haukuwa na mafanikio mbele ya lango, huku fowadi huyo akistahimili hali duni ambapo alifunga mabao mawili pekee katika mechi 11 kabla ya mwaka mpya kuanza.

Kutokana na hali hiyo mbaya, uvumi ulianza kuzunguka mustakabali wa muda mrefu wa mshambuliaji huyo huko Barcelona.

Lewandowski amekuwa akihusishwa mara kwa mara kuhamia Saudi Arabia ili kuungana na nyota wenzake wakongwe, Karim Benzema na Cristiano Ronaldo, na Sport wameripoti kwamba alipokea ofa ambayo 'itaongeza mara tatu' mshahara wake wa sasa Barca ili kuhamia Mashariki ya Kati.

Licha ya ofa hiyo nono, ripoti hiyo inaeleza zaidi kwamba Lewandowski ameamua kukataa ili kuona mwaka wa tatu na wa mwisho wa mkataba wake wa sasa pale Barcelona.

Akizungumza hivi majuzi, mshambuliaji huyo alidokeza nia yake ya kubakia Barca kwa kusisitiza kwamba anatamani kucheza tena Camp Nou - huku uwanja huo ukifanyiwa ukarabati mkubwa.

"Ni moja ya malengo, kucheza tena Camp Nou," alisema Lewandowski.

"Ni uwanja mzuri bila shaka tunapaswa kusubiri miezi kumi nadhani. Katika msimu mpya, karibu mwisho wa mwaka, tutakuwa uwanjani na tutaweza kucheza na watu wetu wote na mazingira hayo.



"Ninajisikia vizuri sana mjini, familia yangu pia, nina furaha na furaha sana. Nina furaha katika klabu, lakini pia katika kila kitu kingine."

HABARI MICHEZO

## Benchikha ataja mbinu kuishika Al Ahly Cairo

INATOKA UKURASA 24

lao la huku, mechi itakuwa nzuri zaidi," alisema kocha huyo.

Kuhusu kuwa na dakika 90 ngumu Cairo kutokana na kucheza ugenini mbele ya mashabiki lukuki wa Al Ahly, Benchika alisema timu kubwa kama Simba imeshakuwa moja kati ya zile zinazoogopwa ugenini.

"Simba imeshatoka kwenye zile timu zinazohofia kucheza ugenini, tumeshacheza Cairo, Morocco, Algeria na tumecheza vizuri sana, tutacheza kama tulivyocheza mechi iliyopita, sasa wao ndiyo wataangalia wafanye nini, na kama wachezaji wangu watakuwa watulivu tukapata bao, mechi itakuwa ngumu kwao pia," alisema.

Katika mechi hiyo, Simba inahitaji ushindi kuanzia mabao 2-0 ama 2-1 au 3-2 na kuendelea ili kuweza kutinga nusu fainali, ambayo ndiyo malengo yao makuu msimu huu.

## Yanga yaanika kamati mchakato mabadiliko

INATOKA UKURASA 24

tulipo na kwenda kupata mfumo wa kisasa wa uendeshaji wa mpira," alisema.

Hersi alisema kuna mambo matatu ambayo wameyafanyia kazi ikiwamo eneo la umiliki wa klabu, ambapo nyuma ilikuwa inamilikiwa na wanachama kwa asilimia 100, mfumo mchanganyika ambapo asilimia fulani kumilikiwa na wanachama na taasisi fulani.

"Tulipendekeza asilimia 51 za wanachama na 49 wawekezaji, mfumo wa uongozi wa klabu, kamati ilipendekeza kuwa klabu ilikuwa inaongoza na nguzo moja, baada ya kujifunza na kuja na mifumo ya nguzo tatu ili moja ibaki kama ilivyokuwa kwa kamati ya utendaji.

"Ya pili mfumo wa kutengeneza kampuni mpya itakayojengwa na klabu ambayo itamiliki asilimia 100 ambayo itauza asilimia 49 kwa wawekezaji, kampuni itaundwa na watu tisa na kutoa wawakilishi watano kutoka kwa klabu na watakaonunua watatoa wanne," alisema Hesri.

Aliongeza kuwa mwenyekiti atatoka katika klabu ambaye atakuwa ni rais, na mtu wa pili atatoka katika baraza la wadhamini na watatu atakuwa katibu mkuu ambaye ataajiriwa na wala si mtendaji mkuu.

"Baada ya yote hayo chini ya bodi hiyo itakuwa na mtendaji mkuu, hivyo yule CEO wa klabu atatoka katika klabu na kwenda katika bodi ya kampuni ambayo itaendesha shughuri zote za klabu," alisema Hersi.

# DILUNGA AREJEA UWANJANI BAADA YA MIEZI MITANO

**Na Adam Fungamwango**

WINGA wa timu ya JKT Tanzania, Hassan Dilunga, ameanza mazoezi na timu hiyo baada ya kukaa nje takriban miezi mitano kutokana na majeraha.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo jana, imeeleza kuwa mchezaji huyo ameanza mazoezi na anatarajia kuitumikia timu hiyo kwenye mechi zijazo za Ligi Kuu, ambapo huenda akawa mmoja wa wachezaji watakaoshuka dimbani katika mechi kati ya timu hiyo dhidi ya Tabora United, Aprili 14, mwaka huu, itakayopigwa Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mjini Tabora.

**Msemaji wa klabu hiyo, Masau Bwire, amesema kurejea kwa Dilunga ni faraja kwa klabu, kwani wana uhakika ataleta chachu kutokana na uwezo mkubwa alionao.**

"Madaktari wamesema sasa amepona, tuna imani atakuja kuibadilisha timu, ni mchezaji mkubwa na mzoefu," alisema Bwire.

Dilunga, ambaye kabla ya kujiunga na timu hiyo alitokea Klabu ya Simba, amekuwa akisumbuliwa mara kwa mara na majeraha, na hata alipokuwa kwenye klabu hiyo ya awali alikaa kwa muda wa miezi kadhaa nje kwa sababu hiyo, kabla ya kupona na baadaye kutimkia JKT Tanzania.

Akiwa na JKT Tanzania, Dilunga alipata majeraha kwa kuumizwa na Mtenje Albano wa Dodoma Jiji fc, kwenye Uwanja wa Chamazi katika mechi ya Ligi Kuu iliyochezwa Oktoba 23, mwaka jana, tangu hapo amekuwa nje ya uwanja kwa matibabu kwa zaidi kwa miezi mitano, ambapo yalifanyika nchini Afrika Kusini.

Timu hiyo haipo kwenye nafasi nzuri ya msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa nafasi ya 15 kwa pointi 20 baada ya kucheza mechi 20.




Mshambuliaji wa Arsenal, Gabriel Jesus (kushoto) na straika wa Manchester City, Erling Haaland, wakiwania kumiliki mpira kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Etihad na kumalizika kwa sare tasa. **PICHA: MTANDAO**

# *Dau la Fei Toto latajwa*

**Na Saada Akida**

KLABU ya Azam, imeweka wazi dau wanalolitaka kwa timu inayohitaji huduma ya kiungo mshambuliaji wao, Feisal Salum 'Fei Toto', kuwa ni dola za Kimarekani milioni mbili sawa na Sh. bilioni 5.1 za Tanzania.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Azam FC, Hashim Ibwe, alisema hawajatangaza kumuuza Fei Toto, lakini kama kuna klabu inamhitaji, italazimika kuvunja mkataba wake kwa kipindi kilichobakiwa, amabao una thamani ya dola za Kimarekani milioni mbili.

Alisema wamekuwa na utamaduni mzuri wa kuwauza wachezaji wao endapo kuna timu inahitaji mchezaji ndani ya klabu yao na wameshafanya hivyo mara kadhaa hapo nyuma.

"Hatujawahi kuwa wachoyo na mtu ambaye ana mhitaji mchezaji hapa Azam FC, kwa sababu tumekuwa na wachezaji na kuwaacha na kwenda katika klabu mbalimbali wakiwamo Aishi (Manula), Kapombe (Shomari), Erasto (Nyoni), Mudathir (Yahya) na Salum Aboubakar.

"Hatujatangaza ofa juu ya Fei Toto bali kama kuna klabu ambayo inamhitaji kiungo huyo tunawakaribisha waje mezani, tumepiga hesabu na kuona thamani ya mkataba wa mchezaji huyo ni kuona sawa na kiasi hicho," alisema Ibwe.

Kuna taarifa kuwa Fei Toto ameanza kutajwa katika klabu mbalimbali ikiwamo moja kubwa hapa nchini.

# Michezo

Jumanne Aprili 2, 2024

Nipashe




Klopp akunwa na bao la Salah UKURASA 22

# Benchikha ataja mbinu kuishika Al Ahly Cairo

## Apanga kujilipua, asema watapeleka moto mwanzo mwisho huku...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI akiendelea kukisuka kikosi chake kuelekea mechi ya marudiano ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly itakayopigwa Uwanja wa Cairo, Misri Ijumaa wiki hii, Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, ametaja mbinu zinazoweza kuwasaidia kupindua matokeo nchini humo kama wachezaji wataweza kuzitekeleza uwanjani.

**Simba inakibarua kigumu cha kupindua matokeo ya bao 1-0, ililoruhusu Ijumaa iliyopita katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, ambapo inatakiwa kupata ushindi zaidi ya huo ili kutimiza malengo yao ya kutinga nusu fainali ya michuano hiyo mikubwa zaidi kwa ngazi ya klabu barani Afrika.**

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Benchikha alisema mbinu pekee ya ushindi nchini Misri Ijumaa wiki hii ni kuishambulia Al Ahly mfululizo kiasi cha kuwatia hofu, huku akitabiri utakuwa ni mchezo wa kupishana zaidi.

Kocha huyo alisema kama kwenye mechi ya kwanza hapa nchini walicheza kwa kujihami zaidi, lakini walifanikiwa kuingia ndani ya eneo lao la hatari zaidi ya mara saba, huku wachezaji wake wawikikosa mabao mengi, ana uhakika wanaweza kufanya zaidi ya mara hizo.

Kocha huyo alisema mfumo atakaocheza akiwa ugenini hautotofautiana na alioutumia Ijumaa iliyopita, ila kuna vitu ambavyo atawaongezea wachezaji wake ili kuwafanya wawe hatari zaidi wanapokuwa langoni.

Alisema kwa jinsi alivyoiangalia Al Ahly ni timu inayofikika kirahisi langoni mwao hata kama wanacheza kwa kujihami, na anaamini katika mechi ya



Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha

marudiano hawatofanya hivyo, hivyo wataachia mianya mingi na nafasi.

"Hatuna cha kupoteza, tunaenda kushambulia Cairo, tutajaribu bahati yetu, inawezekana huko tutapata mabao, kwa nini isiwezekane?

"Mimi ni kocha na hii ni kazi yangu kwa miaka mingi, nimeshafundisha timu kubwa na zikacheza mechi kubwa zaidi kwa hiyo hata mechi hii ya marudiano tunacheza kwa ajili ya kushinda bila kuhofia chochote. Kama kufungwa tumeshafungwa, tutacheza kama fainali, ninachotaka na kuwaambia wachezaji wangu ni kwamba wapinzani wetu ndiyo wawe na hofu na si sisi, na tukifanikiwa kupata bao la kulifuta

INAENDELEA UKURASA 23

# Yanga yaanika kamati mchakato mabadiliko

**Na Saada Akida**

KLABU ya Yanga imeteua kamati ya watu wanne, inayoongozwa na Mwenyekiti Alex Mgongola kuendelea kusimamia sehemu iliyosalia ya mchakato wao wa mabadiliko, imeelezwa.

Wajumbe walioteulizwa watakaokuwa chini ya Mgongolwa, ni Raymond Wawa , Ivan Torino na Eliakim Maswi, ambao watasimamia mchakato huo unaolezwa kubakia sehemu chache kukamilika.

Rais wa Yanga, Mhandisi Hersi Said, akizungumza na Nipashe jana makao makuu ya klabu hiyo, alisema maendeleo ya mfumo wa mabadiliko ambayo ni kiungo kikubwa cha kwenda katika mafanikio yanapaswa kukamilika mapema sasa.

Alisema kwa kipindi chote walifanikiwa katika mchakato huo na kupiga hatua kubwa na wanaimani kamati hiyo itamalizia sehemu iliyosalia na wanatarajia watakaoingia katika bodi kila mmoja atakuwa na haki.

"Hatua tunayoendea sasa ni kufungua kampuni, kufanya tathimini ya mali za klabu ambayo tutaangalia itatoa vitu gani kuja kwenye kampuni na kuhusu kuuza utaratibu wa hisa," alisema Hersi.

Alifafanua kuwa baada ya mchakato watatoka wajumbe watano katika klabu kwa ajili ya kuuza asilimi 49 na hatua ya mwisho ambayo imefanyika ni kuhamisha majukumu yao kwenda katika bodi.

"Kwenye hizo hisa 49, hakuna mtu mmoja kumiliki na lazima wawe watu wanne na kila mmoja atapata 12.25, kwenye bodi itakuwa na watu tisa ambapo watano wanatoka klabuni na wawekezaji wanatoa wanne," alisema rais huyo.

Aliongeza kuwa baada ya kukamilika kwa mchakato huo wanatarajia mafanikio makubwa ndani ya klabu hiyo kwa siku za usoni kwa kuwa itakuwa inaendeshwa kisasa.

Hersi alisema Yanga ndiyo klabu kogwe ndani ya taifa hili na kwa heshima hiyo, inepitia safari ndefu milima na mabado hadi kufikia mafanikio yaliyopo sasa.

Alisema kuwapo kwa wanachama wengi au mashabiki ni thamani ya uwapo watu hao, na kwamba kipindi cha nyuma kulikuwa na Yusuph Manji alipambana kuifikisha Yanga katika mafanikio, lakini baada ya kupata changamoto mambo yote yakasimama.

"Hilo lilikuwa funzo na kuna watu wakafikiria kuweza kuondoa katika mfumo wa klabu kuendeshwa kizamani na kwenda kisasa kipindi hicho alikuwapo Mwenyekiti Mshindo Msola.

"Aliunda kamati na ilifanya kazi kubwa ya kutafuta elimu na wataalum ili kupata mafunzo ya kuweza kutuondoa hapa

INAENDELEA UKURASA 23



Rais wa Yanga, Mhandisi Hersi Said

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >